# HAZINA YETU

TOLEO LA TANO 2025 | ISSN: 3108-8597









# JARIDA LA HAZINA YETU TOLEO LA TANO



# Neno la Katibu Mkuu

Kwa mara nyingine, ninayofuraha kwamba Jarida la Hazina Yetu, Toleo la Tano, limechapishwa. Jarida letu hili linaloangazia mwenendo wa kiuchumi na kifedha wa nchi yetu, limejikita katika kutoa taarifa na tafakuri ya kina kuhusu maendeleo ya uchumi wa Taifa katika Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2025/26, likibainisha mafanikio yaliyopatikana, changamoto, na mwelekeo wa mbele katika utekelezaji wa sera za kifedha na kiuchumi.

Kwa kipindi cha Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2025/26, uchumi wa Taifa umeendelea kuwa imara licha ya changamoto za kiuchumi duniani. Takwimu zinaonyesha kuwa ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) umeendelea kwa kasi ya takriban 5.4 % kwa mwaka katika Robo hii ya kwanza. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na sekta za madini (16.6%), huduma za fedha na bima (15.4%) pamoja na uzalishaji wa umeme ambao uliongezeka kwa takriban 19.0%. Sekta ya kilimo nayo iliongezeka kwa takriban 3.0% katika kipindi hicho.

Mfumuko wa bei umeendelea kubakia katika kiwango cha chini kinachoweza kudhibitiwa cha wastani wa 3.2%., ukichangiwa na upatikanaji mzuri wa bidhaa muhimu na utekelezaji makini wa sera za fedha na bajeti. Hali hii imechangia kuimarika kwa uwezo wa wananchi katika kukidhi mahitaji yao ya kila siku na kuendeleza shughuli za uzalishaji.

Sekta ya fedha nayo imeendelea kuwa thabiti, ikiwa na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kupanuka kwa huduma za kifedha jumuishi, na kuimarika kwa mfumo wa benki nchini. Mageuzi katika matumizi ya teknolojia za kifedha (FinTech) yameendelea kuongeza ufanisi na upatikanaji wa huduma kwa wananchi na wafanyabiashara wadogo.

Kwa ujumla, mafanikio haya ni matokeo ya utekelezaji thabiti wa sera za Serikali, ushirikiano wa wadau wa maendeleo, sekta binafsi, na wananchi kwa ujumla. Tunapoendelea na mwaka wa fedha 2025/26, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, kukuza uchumi jumuishi, na kuhakikisha ustawi wa Watanzania wote.

Viongozi wa Wizara ya Fedha wameendelea kutekeleza jukumu lao muhimu la kuratibu mahusiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau wa maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi.

Wizara, kupitia uongozi wake wa juu, imefanya mikutano kadhaa na mashirika ya kimataifa, taasisi za kifedha, na balozi za nchi rafiki kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kifedha na kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini.

Mikutano hiyo imekuwa jukwaa muhimu la kujadili vipaumbele vya maendeleo vya taifa, ikiwemo uboreshaji wa miundombinu, huduma za jamii, na kukuza uchumi jumuishi.

Aidha, katika kipindi hicho, Wizara ya Fedha imesaini mikataba kadhaa ya mikopo nafuu na misaada kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo. Baadhi ya mikataba hiyo imehusisha Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW), Washirika wa Maendeleo wanaochangia Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), ikilenga kusaidia utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama uboreshaji wa huduma za maji, afya, na elimu.

Viongozi wa Wizara ya Fedha pia wamekutana na wawakilishi wa sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kujadili fursa za ubia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP).

Mazungumzo hayo yalilenga kuvutia uwekezaji zaidi katika sekta za uzalishaji, ujenzi wa miundombinu, na nishati jadidifu, sambamba na kuimarisha mazingira rafiki ya biashara. Mazungumzo hayo yameonesha dhamira ya Serikali ya kuhakikisha wadau wote wanashiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa taifa.

Viongozi wa Wizara ya Fedha wameendelea kutekeleza jukumu lao muhimu la kuratibu uhusiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau wa maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi katika nyanja za kiuchumi.

**Dkt. Natu El-maamry Mwamba**
**Katibu Mkuu Wizara ya Fedha**



# Neno la Mhariri Mkuu

***Wapendwa wasomaji,***

Karibu sana kwenye Toleo la Tano la Hazina Yetu, Jarida letu rasmi la Wizara ya Fedha linalolenga kuwafahamisha, kuwahamasisha na kuwaunganisha Watanzania kupitia taarifa sahihi, za kina na zenye kuelimisha kuhusu shughuli mbalimbali za kifedha, kiuchumi na kijamii zinazotekelezwa na Wizara.

Katika toleo hili jipya, tumekuletea maudhui yenye mvuto na taarifa za kina zinazogusa moja kwa moja maendeleo ya nchi yetu. Kwenye Sehemu ya Makala, utasoma kwa kina kuhusu masuala ya kiuchumi, usimamizi wa fedha za umma, mageuzi ya mifumo ya kifedha, na taarifa za mafanikio zinazohamasisha. Kila makala imeandikwa kwa ustadi mkubwa na wataalamu wetu ili kukupa maarifa mapya na mtazamo mpana juu ya maendeleo ya kifedha nchini.

Pia Sehemu ya Matukio Yaliyojiri, utapata taarifa muhimu kuhusu shughuli na mikutano mbalimbali ya Wizara na taasisi zake, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha hivi karibuni.

Tunakualika pia kutembelea Kona ya Maonesho ya Sabasaba na Nane Nane, ambapo tumekuandalia yaliyojiri katika maonesho hayo hasa taarifa zinazoangazia ushiriki wa Wizara ya Fedha na taasisi zake katika maonesho hayo muhimu, pamoja na ubunifu na huduma zilizowavutia wananchi wengi.

Usikose pia Sehemu ya Kamera Yetu, inayokuletea picha nzuri na zenye ubora wa hali ya juu, zikionesha matukio muhimu, nyuso za watumishi wetu wenye bidii, na mafanikio halisi ya kazi za Wizara kwa njia ya picha.

Tunatambua mchango mkubwa wa wasomaji wetu katika kutuongoza kuboresha Jarida hili. Hivyo, tunakukaribisha uendelee kutusoma, kutoa maoni na kushiriki nasi katika safari hii ya kuelimisha, kuhabarisha na kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi ya taifa letu.

Tukutane ndani ya kurasa hizi zenye maarifa, ubunifu na hamasa ya maendeleo.

Kwa niaba ya Timu ya Uhariri,

Benny Mwaipaja
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Wizara ya Fedha




# MAKALA

MAKALA






# DIRA YA MAENDELEO 2050 NA HARAKATI ZA KUIMARISHA UCHUMI ENDELEVU WA TANZANIA

*Na Ramadhani Kissimba*

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni mpango thabiti, jumuishi na wenye maono ya mbali, unaoakisi matarajio ya pamoja na mwelekeo wa kimkakati kwa kipindi cha miaka 25 ijayo, Dira hii inakusudia kuboresha hali ya maisha ya Watanzania kupitia ushirikishwaji wa wananchi na mipango ya maendeleo endelevu.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua umuhimu wa maono na matarajio ya Watanzania katika kufikia malengo hayo, hivyo ikaona haja ya kuwashirikisha wananchi kutoa maoni yao katika Dira ya Taifa ya maendeleo 2050.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, jijini Dodoma, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisema Serikali inaendelea na kazi ya kukuza uchumi, kuwezesha wanawake na vijana, kupanua wigo wa washiriki na wadau mbalimbali wa maendeleo na sekta binafsi, na kusukuma mbele mageuzi ya kisera na ya kijamii yatakayoleta mafanikio kwa wote.



> *Serikali imejikita katika kuimarisha uchumi jumuishi na shindani, unaogusa maisha ya kila Mtanzania, kutoka mijini hadi vijijini" alisema Dkt. Samia.*

Malengo makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni kukuza Uchumi, Kuimarisha uchumi wa viwanda na kuongeza uzalishaji, Kuhakikisha usawa, Kuweka mazingira bora ya kijamii na kiuchumi kwa kila Mtanzania, Kujenga utawala bora, Kuimarisha demokrasia na utawala wa Sheria.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni mwendelezo wa Mipango na Mikakati mbalimbali ya Serikali iliyoelekezwa katika awamu tofauti kwa lengo la kupambana na maadui watatu wa maendeleo (ujinga, maradhi na umasikini) na kuinua hali ya maisha ya wananchi.

Dira 2050 inaweka bayana azma ya kuendeleza mafanikio yaliyotokana na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa kuifikisha

Tanzania kwenye ngazi ya juu ya maendeleo na kuwa nchi yenye uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu utakaongozwa na maendeleo ya viwanda ambapo matarajio ni kwamba ifikapo mwaka 2050 pato la Taifa litakuwa lenye thamani ya dola za Marekani trilioni moja na wastani wa pato la mtu mmoja litakuwa na thamani ya dola za Marekani 7,000.

Kupitia nguzo kuu za Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambazo ni uchumi imara, jumuishi na shindani, Uwezo wa watu na maendeleo ya jamii, uhifadhi wa mazingira, ustahimilivu wa maendeleo ya tabianchi pamoja na matarajio yaliyoanishwa katika nguzo hizo, Serikali kupitia Wizara za Kisekta kwa kushirikiana na sekta binafsi ina jukumu kubwa katika kutengeneza mazingira ya kufanikisha yale yote yaliyolengwa na kuanishwa na Dira 2050

Uchumi imara, jumuishi na shindani ni moja ya nguzo kuu ya kujenga Taifa lenye ustawi, kwani nguzo hii inafungua fursa za kiuchumi na hivyo kuweka mazingira ya kupunguza umaskini na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wote.

Uchumi imara utahakikisha kwamba maendeleo ya kiuchumi yanakuwa na taswira chanya kwa jamii na kuwanufaisha wananchi wote. Katika muktadha huu, Tanzania imeendelea kupiga hatua za kiuchumi, ambapo uchumi umeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.2 kwa mwaka katika kipindi cha miongo miwili iliyopita.

Katika bajeti ya mwaka 2025/26 ambayo iliandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063, Malengo ya Maendeleo endelevu 2030 pamoja na miongozo mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda, Serikali imetenga takribani Shilingi trilioni 17.5 sawa na 31% ya bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ikilenga kuimarisha sekta za kimkakati zinazohusiana moja kwa moja na utekelezaji wa Dira 2050.

Sekta ya Elimu na Afya pia imepewa kipaumbele, ambapo shilingi bilioni 7,394.4 zimetengwa kwa ajili ya elimu na shilingi bilioni 3,009.2 kwenye sekta ya afya kwa mwaka wa fedha 2025/26 hatua inayolenga kuboresha rasilimali watu na huduma za jamii ili kuhakikisha wananchi wote wanashiriki kikamilifu katika shughuli za kukuza Uchumi na kila mwananchi kunufaika na matunda ya ukuaji wake.

Ili kufanikisha malengo ya Dira 2050, ni lazima kujenga Uchumi mseto, shirikishi na shindani wa Kimataifa. Uchumi huu utategemea rasilimali za ndani na kuendeshwa kwa misingi ya sera madhubuti na mifumo bora ya udhibiti inayochochea ukuaji wa biashara na ujasiriamali, kurasimisha sekta isiyo rasmi na kuvutia uwekezaji mkubwa wa ndani na nje ya nchi.

Uchumi jumuishi sio kujenga tu uchumi wenye ukuaji mkubwa, bali ni kuhakikisha kwamba ukuaji huo unawanufaisha watu wote, unapanua fursa kwa makundi yote ya jamii, kuondoa umasikini na unalinda mazingira kwa vizazi vijavyo. Aidha Uchumi jumuishi utaongeza Pato la Taifa lakini pia utaondoa pengo la kipato na huduma kati ya makundi na maeneo tofauti.

Sekta ya Elimu na Afya pia imepewa kipaumbele, ambapo shilingi bilioni 7,394.4 zimetengwa kwa ajili ya elimu na shilingi bilioni 3,009.2 kwenye sekta ya afya kwa mwaka wa fedha 2025/26 hatua inayolenga kuboresha rasilimali watu na huduma za jamii ili kuhakikisha wananchi wote wanashiriki kikamilifu katika shughuli za kukuza Uchumi na kila mwananchi kunufaika na matunda ya ukuaji wake.

Ili kufanikisha malengo ya Dira 2050, ni lazima kujenga Uchumi mseto, shirikishi na shindani wa Kimataifa. Uchumi huu utategemea rasilimali za ndani na kuendeshwa kwa misingi ya sera madhubuti na mifumo bora ya udhibiti inayochochea ukuaji wa biashara na ujasiriamali, kurasimisha sekta isiyo rasmi na kuvutia uwekezaji mkubwa wa ndani na nje ya nchi.

Uchumi jumuishi sio kujenga tu uchumi wenye ukuaji mkubwa, bali ni kuhakikisha kwamba ukuaji huo unawanufaisha watu wote, unapanua fursa kwa makundi yote ya jamii, kuondoa umasikini na unalinda mazingira kwa vizazi vijavyo. Aidha Uchumi jumuishi utaongeza Pato la Taifa lakini pia utaondoa pengo la kipato na huduma kati ya makundi na maeneo tofauti.

***Mwisho***





# IJUE WIZARA YA FEDHA

*Na Eva Valerian Ngowi*

Katika jitihada za kuendelea kuwapatia wasomaji wetu uelewa mpana kuhusu majukumu, muundo na mchango wa Wizara ya Fedha katika kusimamia uchumi wa Taifa, Jarida hili linaendeleza mfululizo wa makala zilizotangulia ambazo zilijikita katika historia ya Wizara tangu kupata Uhuru hadi sasa, sambamba na maelezo ya Idara sita ambazo ni Idara ya Uchambuzi wa Sera, Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali, Idara ya Fedha za Nje, Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali, Idara ya Sera za Ununuzi wa Umma, na Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha.

Katika makala haya, tunazidi kuwaeleza wasomaji wetu kwa undani kuhusu idara nyingine tatu zinazocheza nafasi ya kipekee katika kuhakikisha usimamizi thabiti wa rasilimali fedha za umma na uboreshaji wa mifumo ya kiutendaji ndani ya Serikali. Idara hizi ni Idara ya Menejimenti ya Mifumo ya Fedha na Huduma za TEHAMA, Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali, na Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali.

Kupitia makala haya, msomaji atapata fursa ya kufahamu namna idara hizi zinavyochangia katika kuimarisha uwajibikaji, uwazi, ufanisi na matumizi bora ya teknolojia katika usimamizi wa fedha za umma, sambamba na jukumu lao la kuhakikisha Serikali inatekeleza majukumu yake kwa weledi na kwa manufaa ya wananchi wote.

## 1 Idara ya Menejimenti ya Mifumo ya Fedha na Huduma za TEHAMA (FISM)

Katika dunia ya sasa inayosukumwa na kasi ya maendeleo ya teknolojia, matumizi ya TEHAMA yamekuwa chachu muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma serikalini. Kabla ya ujio wa mifumo ya kielektroniki, wananchi walikumbana na changamoto nyingi katika kufanya malipo ya huduma mbalimbali za serikali kama vile umeme, maji, ardhi na usafiri. Ili kulipia huduma hizo, ililazimu kufika katika ofisi husika au kwa mawakala, jambo lililosababisha foleni ndefu, upotevu wa muda, na wakati mwingine usumbufu kwa wananchi.

Kutokana na changamoto hizo, Wizara ya Fedha ilichukua hatua madhubuti kwa kuanzisha mfumo wa Government e-Payment Gateway (GePG)- mfumo wa kisasa wa TEHAMA uliobuniwa na Idara ya Menejimenti ya Mifumo ya Fedha na Huduma za TEHAMA (FISM) ili kurahisisha na kuratibu malipo yote ya serikali kwa njia ya kielektroniki. Kupitia GePG, sasa wananchi wanaweza kufanya malipo ya huduma mbalimbali wakiwa popote na kwa wakati wowote, kwa kutumia simu, kompyuta au huduma za kibenki mtandaoni.

Idara hii ina dhamana ya kuhakikisha kuwa mifumo yote ya kifedha ya Serikali inaendeshwa, inalindwa na kuendelezwa kwa viwango vya juu vya kitaalamu na kiteknolojia, ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma.

Utekelezaji wa mfumo huu umeleta mageuzi makubwa katika ukusanyaji wa mapato ya serikali kwa kuongeza uwazi, ufanisi, na usalama wa miamala ya kifedha. Kwa hakika, GePG imekuwa nguzo muhimu katika safari ya kuelekea serikali ya kidijitali, inayoweka kipaumbele katika utoaji wa huduma bora, rahisi na za kisasa kwa wananchi.

Makala haya yanafafanua kwa kina majukumu ya idara hii na mchango wake katika kuhakikisha ufanisi wa mifumo ya kifedha na TEHAMA serikalini.

## Lengo Kuu la Idara

Lengo kuu la Idara ya FISM ni kutoa utaalamu na huduma za kisasa katika maendeleo na uendeshaji wa mifumo ya kifedha serikalini. Hii inalenga kuhakikisha kuwa Mifumo ya TEHAMA inayosimamia fedha za Serikali ni salama, ya kuaminika, na inayoendeshwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kufanikisha utoaji wa huduma bora kwa umma.



**DKT. JOHN SAUSI**

MKURUGENZI WA IDARA YA USIMAMIZI WA MIFUMO YA FEDHA NA HUDUMA ZA TEHAMA

## Majukumu ya Idara

### 1 Kuandaa Sera na Miongozo ya Usalama wa TEHAMA kwa Mifumo ya Kifedha ya Serikali.

Idara huandaa sera, taratibu na miongozo ya usalama inayolinda mifumo ya kifedha dhidi ya udukuzi, upotevu wa data au majanga ya kimazingira, kuhakikisha taarifa nyeti za kifedha zinalindwa ipasavyo.

### 2 Kuendeleza, Kutekeleza na Kuhifadhi Mifumo ya Kifedha ya Serikali

Mifumo kama MUSE, GePG, CBMS, GAMIS, TPPS na mingineyo ambayo ni Mifumo tegemezi ya Serikali katika usimamizi wa bajeti, matumizi na mapato. Idara husimamia kubuni, kusimika, kuhuisha na kuhifadhi mifumo hiyo ili kuhakikisha inafanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu.

### 3 Kutoa Msaada wa Kiufundi kwa Wizara, Idara, Wakala na Serikali za Mitaa

Idara hutoa msaada wa haraka wa kiufundi kwa taasisi za Serikali zinapokumbana na changamoto katika matumizi ya Mifumo ya kifedha, ili kuepusha ucheleweshaji wa shughuli muhimu kama malipo, upangaji wa bajeti na ukusanyaji wa mapato.

### 4 Kutekeleza na Kusimamia Mifumo ya TEHAMA Ndani ya Wizara ya Fedha

Aidha, idara inasimamia mifumo ya ndani ya Wizara ya Fedha ikiwemo mitandao ya mawasiliano, barua pepe, hifadhi ya data na vifaa vya TEHAMA, kuhakikisha shughuli za wizara zinafanyika kwa ufanisi na usalama.

## Faida za Uwepo wa Idara hii

Usimamizi Imara wa Fedha za Umma: Hutoa urahisi wa ufuatiliaji na udhibiti wa matumizi ya fedha serikalini.

Uwazi na Uwajibikaji: Huhakikisha kumbukumbu sahihi na ufuatiliaji wa taarifa za kifedha kwa wakati.

Ufanisi na Uokoaji wa Gharama: Hupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuongeza kasi ya utoaji wa huduma.

Ulinzi wa Taarifa: Kupitia sera za usalama, hupunguza hatari ya wizi au upotevu wa data.

## 2 Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMD)

Usimamizi wa mali za Serikali nchini Tanzania umeainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kifungu cha 27(1). Aidha, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amemkabidhi Waziri wa Fedha jukumu la kusimamia mali za umma kupitia Hati ya Majukumu ya Waziri (Instrument).

Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348, Katibu Mkuu Hazina amepewa jukumu la kusimamia mali za umma, na utekelezaji wa jukumu hili unafanywa na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMD). Idara hii ilianzishwa mwaka 2008/2009 ikitokana na iliyokuwa Idara ya Uhakikimali (Stock Verification Department) iliyoanzishwa kabla ya Uhuru mwaka 1956.

Licha ya majukumu ya Idara hii, kila Afisa Masuuli na Mkuu wa Taasisi za Umma ana wajibu wa kuhakikisha mali za Serikali zinapatikana kwa njia sahihi, zinatumika kwa manufaa ya umma, zinatunzwa na taarifa zake zinahifadhiwa ipasavyo.



**BW. CHOTTO SENDO**
MKURUGENZI WA IDARA YA USIMAMIZI WA MALI ZA SERIKALI

ya TEHAMA inayosimamia fedha za Serikali ni salama, ya kuaminika, na inayoendeshwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kufanikisha utoaji wa huduma bora kwa umma.

### Majukumu ya Idara

1. Kuandaa na kupitia sera, sheria, kanuni, miongozo na taratibu zinazohusu upatikanaji, utunzaji na uondoshaji wa mali za umma.
2. Kufuatilia utekelezaji wa sera na viwango vya kimataifa kuhusu usimamizi wa mali za umma.
3. Kushughulikia ajali, potevu na fidia zinazohusiana na mali za umma.
4. Kusimamia waendesha minada na udalali.
5. Kusimamia Daftari Jumuifu la Mali za Umma (Centralized Assets Register).

### Muundo wa Idara

A. Sehemu ya Ajali na Fidia

- Kushughulikia madai ya fidia na kifuta machozi kutokana na ajali au amri za mahakama.
- Kufuatilia uharibifu wa mali za umma na tozo kwa waliosababisha hasara.
- Kufanya ukaguzi maalum wa magari, mitambo na mali nyingine za Serikali.

B. Sehemu ya Mifumo ya Usimamizi wa Mali

- Kuandaa na kusimamia mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa mali.
- Kufanya uhakiki wa mali katika taasisi mbalimbali za umma.
- Kutoa vibali vya usajili wa vyombo vya moto vya Serikali (ST, PT, UT, MT, DFT).
- Kushughulikia mali zilizotaifishwa au zilizorudishwa kwa Katibu Mkuu Hazina.
- Kusimamia uondoshaji wa mali, waendesha minada na madalali.
- Kushauri juu ya uhamisho wa mali na ubomoaji wa majengo ya Serikali.

Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali ni kiungo muhimu kinachohakikisha rasilimali za umma zinadhibitiwa, zinatunzwa na zinatumika kwa manufaa ya Watanzania wote. Kupitia mifumo ya kisasa ya usimamizi, idara hii inaboresha uwajibikaji, ufanisi na udhibiti wa mali za Serikali, sambamba na kukuza uwazi na uwajibikaji katika sekta ya umma.

## 3 Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (IAG)

Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (IAG) ni moja ya nguzo muhimu chini ya Wizara ya Fedha yenye jukumu la kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za umma kupitia huduma za ukaguzi wa ndani.

Idara hii inaimarisha ufanisi, uwazi, uwajibikaji na utawala bora katika sekta ya umma kwa kusaidia Serikali kufikia malengo yake ya maendeleo.

### Lengo Kuu la Idara

Lengo kuu la IAG ni kutoa huduma huru na za kitaalamu za ukaguzi wa ndani na ushauri wa kisera unaolenga kuongeza thamani katika utendaji wa sekta ya umma. Idara hufanya kazi kwa uhuru wa kitaaluma, ikizingatia viwango vya taaluma ya ukaguzi wa ndani, ili kubaini mapungufu na kupendekeza maboresho yenye tija kwa Serikali.



**BW. BENJAMIN MAGAI**

MKAGUZI WA NDANI MKUU WA SERIKALI (IAG)

### Majukumu ya Idara

1. Kuandaa na kupitia sera, miongozo na mikakati ya ukaguzi wa ndani.
2. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miongozo hiyo katika taasisi za umma.
3. Kuhakikisha udhibiti na uwajibikaji wa fedha na mali za Serikali.
4. Kuchambua ripoti za ukaguzi na kuziwasilisha kwa Mlipaji Mkuu.
5. Kufanya tathmini ya viashiria vya hatari katika taasisi za umma.
6. Kuandaa na kutekeleza mpango kazi wa ukaguzi wa kila mwaka.
7. Kufuatilia utekelezaji wa bajeti za taasisi za Serikali.
8. Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi.
9. Kufanya ukaguzi maalum na uchunguzi wa matumizi ya fedha au mali.
10. Kutoa mapendekezo ya kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato.
11. Kusimamia ubora wa wataalamu wa ukaguzi na kamati za ukaguzi.
12. Kushauri Kamati za Kudumu za Bunge (PAC & LAAC) kuhusu masuala ya ukaguzi na uwajibikaji.

Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali ni chombo muhimu katika kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali za umma na kuongeza uwajibikaji serikalini. Kupitia kazi zake za ukaguzi na ushauri wa kitaalamu, idara hii huchangia kwa kiasi kikubwa katika kujenga mifumo imara ya udhibiti wa ndani, kupunguza mianya ya rushwa na ubadhirifu, na kukuza utawala bora.

Ili kuendelea kuongeza ufanisi, kuna umuhimu wa kuimarisha uwezo wa wataalamu wa ukaguzi, kutumia teknolojia za kisasa, na kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za Serikali. Hatua hizi zitahakikisha kuwa Tanzania inaendelea kusimamia rasilimali zake kwa uwazi, ufanisi na kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kwa ujumla, idara hizi tatu- Idara ya Menejimenti ya Mifumo ya Fedha na Huduma za TEHAMA (FISM), Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMD), na Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (IAG) zinaunda nguzo imara zinazoiwezesha Wizara ya Fedha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, uwazi na weledi. Kila idara, kwa nafasi yake, inachangia katika kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinasimamiwa kwa usahihi, mifumo ya kifedha inafanya kazi kwa ufanisi, na fedha za wananchi zinatumika kwa manufaa ya maendeleo ya taifa.

Kupitia kazi zao, Serikali inaendelea kujenga misingi thabiti ya uwajibikaji wa kifedha, utawala bora, na matumizi sahihi ya teknolojia ya kisasa katika uendeshaji wa shughuli zake. Hili si tu linasaidia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi, bali pia linaimarisha imani ya umma na wadau wa maendeleo katika usimamizi wa rasilimali za taifa.

Kadri dunia inavyozidi kubadilika kiteknolojia na kiuchumi, Wizara ya Fedha inaendelea kujipambanua kama kinara wa mageuzi ya kiutendaji serikalini mageuzi yanayojikita katika uwazi, uadilifu, ubunifu na matokeo chanya kwa wananchi.

Kwa kuendeleza ushirikiano kati ya idara hizi na taasisi nyingine za umma, pamoja na kuwekeza katika rasilimali watu na teknolojia bunifu, Tanzania itaendelea kuwa na mifumo thabiti, salama na yenye tija katika kusimamia uchumi wake. Hivyo basi, mustakabali wa usimamizi wa fedha na mali za umma uko katika mikono salama yenye dira ya maendeleo endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

***Mwisho***

# UMUHIMU WA MATUMIZI YA NAMBA YA MALIPO (CONTROL NUMBER)






*Na Joseph Mahumi*

Katika kipindi cha hivi karibuni, Serikali ya Tanzania imekuwa ikiboresha mifumo ya ukusanyaji mapato kwa kuanzisha Mfumo Mkuu wa Makusanyo ya Serikali wa Kielektroniki unaojulikana kama Government e-Payment Gateway (GePG), hii ni njia kuu ya makusanyo yote ya Serikali ikiwa na madhumuni ya kuboresha utendaji wake, kuongeza uwazi, kutoa huduma bora kwa wananchi na kurahisisha ulipiaji wa huduma za Serikali.

GePG ina lenga na kuhakikisha malipo ya Serikali yanafanyika kwa urahisi, usahihi, usalama, na kwa ufanisi. Mfumo huu ni Mfumo rasmi wa Serikali ya Tanzania uliobuniwa kwa ajili ya kuratibu na kusimamia malipo yote ya Serikali kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huu unasimamiwa na Wizara ya Fedha. Kupitia GePG, kila malipo yanayotakiwa kulipwa kwa taasisi za Serikali, mfano kulipia umeme, maji, ardhi, n.k, hupitia kwenye njia moja tu (GePG) ya kielektroniki, jambo linalorahisisha usimamizi na ufuatiliaji wa fedha za umma.

Utaratibu wa malipo kupitia GePG ni rahisi na wa moja kwa moja. Mwananchi au taasisi inapohitaji kufanya malipo ya huduma za Serikali, hutengenezewa Ankara au bill yenye Namba ya Malipo (Control Number) ambayo hutumika kama utambulisho maalum.

Baada ya Mwananchi au taasisi kupata Namba ya malipo, atachagua njia ya malipo ambayo itakuwa miongoni mwa njia kadhaa atakazopewa na Mtoa huduma ya Serikali kwa ajili ya kufanya malipo.

Malipo hayo yanaweza kufanyika kupitia benki, mitandao ya simu (USSD na Bank Apps), malipo ya mtandaoni (e-Commece/online payment) kwa kutumia kadi za VISA, MaterCard, UPI, American Express, ATM, au kwa wakala wa malipo waliopo karibu.

Baada ya malipo kukamilika, taarifa husajiliwa moja kwa moja kwenye mfumo na risiti hutolewa, na ujumbe mfupi SMS hutumwa kwa aliyetengenezewa Ankara au bill hivyo kuondoa usumbufu wa kufuatilia uthibitisho wa malipo kwenye ofisi husika.

Hatua hii imeleta mapinduzi makubwa katika usimamizi wa fedha za umma kwa kuwa imeondoa changamoto nyingi zilizokuwepo awali kama vile urasimu, upotevu wa fedha, utata wa kupata taarifa za malipo, udanganyifu, gharama kubwa za ulipiaji huduma, kushindwa kulipa kwa wakati ikiwa benki zimefungwa, kulipa malipo hayohayo zaidi ya mara moja, ugumu wa ufuatiliaji na rushwa. Kwa sasa, kila malipo yanafuatiliwa moja kwa moja kidijitali, jambo linaloongeza uwazi na kuaminika kwa huduma zinazotolewa na Serikali.

Matumizi ya control number yamewasaidia wananchi kupata huduma kwa urahisi mkubwa. Hapo zamani, mtu aliyetaka kulipia huduma fulani kama vile ada ya shule, kodi ya majengo, kiwanja au gharama za pasipoti, ilimbidi kusafiri umbali mrefu kufuata ofisi husika au benki maalum.

Mara nyingine kulikuwa na foleni ndefu na urasimu mwingi ambao ulipoteza muda na kuongeza gharama zisizo za lazima. Hivi sasa, kwa kutumia control number, malipo yanaweza kufanyika kupitia simu ya mkononi (kwa kutumia mitandao ya malipo ya M-Pesa, Tigo Pesa, Airtel Money n.k.) au kupitia benki yoyote iliyo sehemu ya mfumo huu. Hii imerahisisha sana maisha ya wananchi wa vijijini na mijini kwa kuwa hakuna tena haja ya kusafiri mbali ili kulipia huduma za Serikali.

Pili, Mfumo wa control number umeimarisha usalama wa fedha za walipaji na pia mapato ya Serikali. Fedha zote zinazolipwa kwa kutumia namba ya kumbukumbu huelekezwa moja kwa moja katika akaunti ya Serikali iliyokusudiwa. Hii inamaanisha hakuna mtu wa kati anayeweza kuzihodhi au kuzielekeza vibaya kwenye matumizi.

Kwa mfano, mwananchi akilipia ada ya leseni ya biashara, kodi ya majengo ya Serikali, fedha hizo hufika moja kwa moja kwenye mfuko husika wa Serikali bila kupotea njiani. Vilevile, malipo ya kodi ya pango, kodi ya majengo, ada za magari, na gharama za leseni zote zikilipwa kwa njia ya control number, mapato yote hukusanywa bila upotevu wowote. Hii imesaidia Serikali kuwa na uhakika wa mapato yake na kuweza kupanga bajeti vizuri zaidi.

Aidha, kwa sababu kila muamala unahifadhiwa kidijitali, mlipaji anaweza kuthibitisha malipo yake wakati wowote kwa kutumia risiti ya kielektroniki inayotolewa moja kwa moja na Mfumo.

Vilevile, matumizi ya control number yameongeza uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kila malipo yanapopokelewa, taarifa zake zinaonekana mara moja (real time) kwenye mfumo wa Serikali. Hii inarahisisha ukaguzi wa mapato, inapunguza mianya ya rushwa na inawajibisha watumishi wa umma kuhakikisha huduma zinatolewa kwa usahihi na bila upendeleo.

Mwananchi anapolipa kwa kutumia control number, hana hofu ya kudaiwa tena malipo yale yale au kudanganywa kuhusu kiasi anachopaswa kulipa. Mfumo unatoa kiasi halisi na risiti inayotambulika kisheria, jambo ambalo limeongeza imani ya wananchi kwa Serikali yao.

Aidha, faida kubwa nyingine ya Mfumo huu ni kuongeza mapato ya ndani ya Serikali. Kwa kuwa kila malipo sasa yanapitia njia rasmi, Serikali imeweza kuongeza ukusanyaji wa mapato yake kwa kiwango kikubwa.

Fedha hizi hutumika kugharamia miradi ya maendeleo inayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja kama vile ujenzi wa barabara, shule, hospitali, na miradi ya maji.

Mbali na hayo, Mfumo wa Control Number umesaidia sana katika suala la takwimu na taarifa sahihi. Kila muamala unaofanywa kupitia Mfumo huu unarekodiwa na kuhifadhiwa, hivyo Serikali hupata takwimu sahihi za mapato kwa wakati halisi.

*Namba ya Malipo inafanya* ***malipo ya huduma za Serikali*** *kuwa rahisi na haraka*



Takwimu hizi husaidia kupanga bajeti za mwaka, kutathmini mwenendo wa ukusanyaji wa mapato, na kufanya maamuzi ya kisera kwa kuzingatia hali halisi ya mapato. Pia taasisi za Serikali zinaweza kujua huduma ipi inalipiwa zaidi, ni maeneo gani mapato ni madogo, na kuchukua hatua stahiki za kuboresha huduma hizo.

Kwa upande wa wananchi, Mfumo wa Control Number umekuwa msaada mkubwa katika kudhibiti gharama na muda. Mwananchi anapopokea control number, anajua wazi kiasi cha kulipa na njia za kulipa zilizo rahisi kwake. Hii imeondoa changamoto za kutapeliwa na matapeli waliokuwa wakidai malipo yasiyo rasmi.

Aidha, kwa sababu risiti za malipo zinapatikana mara moja, wananchi hupata uhakika wa huduma zao kukamilishwa kwa wakati. Kwa mfano, malipo ya ada ya usajili wa vyeti vya shule, huduma za barabara, au pasipoti hukamilika mara moja baada ya malipo kuthibitishwa.

Kwa ujumla, matumizi ya Namba ya Kumbukumbu ya Malipo (Control Number) ni moja ya mageuzi makubwa zaidi ya namna wananchi wanavyopata huduma za Serikali lakini pia katika usimamizi wa fedha za umma nchini Tanzania.




Mfumo huu umeleta uwazi, usalama, urahisi, usahihi, ufanisi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na ni dhahiri kuwa bila control number, huduma nyingi zingekuwa ngumu, mapato yangepotea, na wananchi wangepoteza muda na fedha nyingi.

Hivyo basi, tuendelee kuutumia Mfumo huu kila mara tunapohitaji kulipia huduma za Serikali, maana control number ni namba ndogo yenye nguvu kubwa kwa maendeleo makubwa ya Tanzania. Usilipe malipo ya Serikali bila kupewa control number, utakuwa umetapeliwa na kuipunguzia Serikali uwezo wake wa kuwahudumia wananchi wake.

***Mwisho***

INSTITUTE OF ACCOUNTANCY ARUSHA

# YOUR TICKET TO EXCELLENCE



**STUDY MASTER'S PROGRAMMES WITH IAA!**

**FOR MARCH AND OCTOBER INTAKE**

- Master of Arts in Peace and Security Studies
- Master of Accountancy
- Master of Accounting and Finance
- Master of Science in Banking and Finance
- Master of Finance and Investment
- Master of Human Resources Management
- Master of Science in Project Planning Management
- Master of Science in Economics and Finance
- Master of Education Management
- Master of Business Administration in Corporate Management
- Master of Business Administration in Information Technology Management
- Master of Business Administration in Leadership & Governance
- Master of Business Administration in Procurement and Supply Management
- Master of Business Administration in Policy Development and Execution
- Master's of Information Security

**For More Details:** www.iaa.ac.tz


### ARUSHA
P.O Box 2798, Njiro Hill, Arusha
Tel: +255 27 2970232
+255 742 833 444
Email: iaa@iaa.ac.tz

### BABATI
P.O. Box 26 Babati, Manyara
Tel: +255 769 107 078
+255 693 035 436
Email: cm_bbt@iaa.ac.tz

### SONGEA
P.O. Box 800 Songea, Ruvuma
Tel: +255 740 284 609
+255 784 481 546
Email: cm_sng@iaa.ac.tz

### DAR ES SALAAM
P.O. Box 69007 Dar es Salaam
Tel: +255 222 864823
+255 714 405 565
Email: cm_dsm@iaa.ac.tz

### DODOMA
P.O. Box 2594 Dodoma
Tel: +255 26 232 3405
+255 782 943 676
Email: cm_dom@iaa.ac.tz

### BUKOMBE
S.L.P 132, Bukombe, Geita
Tel: +255 680 793 575
+255 750 104 113
Email: iaa_bukombe@iaa.ac.tz



# SERIKALI YATHIBITISHA DHAMIRA YA UWAJIBIKAJI KUPITIA MFUMO WA KUPOKEA MAONI

*Na Josephine Majura*



Katika juhudi zake za kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi na wadau mbalimbali kwenye mchakato wa maandalizi ya bajeti ya serikali, Wizara ya Fedha imefanya mageuzi makubwa kupitia kuanzishwa kwa mfumo mpya wa kielektroniki wa kupokea maoni, ujulikanao kama Maoni Portal.

Mfumo huu wa kisasa, uliozinduliwa rasmi mwaka 2023, ni hatua muhimu ya kitaasisi katika kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika kupanga vipaumbele vya taifa kupitia maoni yanayotolewa kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya Serikali.

## Kuondoa Changamoto za Njia za Kawaida

Kabla ya kuanzishwa kwa Maoni Portal, wananchi na taasisi mbalimbali walilazimika kuwasilisha maoni yao kwa njia ya barua au barua pepe.

Njia hii ilikuwa na changamoto nyingi kama vile ucheleweshaji, urasimu, ukosefu wa ufanisi na kutofikika kwa maoni hayo kwa wakati muafaka. Matokeo yake, wananchi wengi, hasa walioko vijijini, walikosa nafasi ya kutoa mchango wao katika maandalizi ya bajeti.

Kupitia Maoni Portal, sasa ni rahisi kwa mtu binafsi, kikundi cha kijamii, taasisi au kampuni kuingia mtandaoni na kuwasilisha mapendekezo yao moja kwa moja, bila hitaji la kupitia kwa mtu wa kati. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha uwazi, ushirikiano, na uwajibikaji wa pamoja katika utungaji na uboreshaji wa sheria pamoja na usimamizi wa fedha za umma.

## Dirisha Maalum la Kupokea Maoni

Mfumo huu wa Maoni Portal huwekwa wazi kwa matumizi kila mwaka kati ya mwezi Novemba hadi Machi, kipindi ambacho Wizara ya Fedha hukusanya maoni sambamba na makongamano ya kodi kikanda na kitaifa kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya Serikali.

Hili ni dirisha muhimu linalotoa nafasi kwa wananchi na wadau kueleza maoni, mapendekezo na mitazamo yao kuhusu sera za kodi, mapato na matumizi ya serikali, huku likiwafanya kuwa sehemu ya maamuzi yanayowagusa moja kwa moja.

### Maeneo Muhimu Yanayopokelewa Kupitia Maoni Portal

Maoni yanayowasilishwa kupitia mfumo huu hujikita zaidi katika maeneo ya msingi kama vile:

- Maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo nchini ili kuongeza ufanisi na uwazi
- Mapendekezo ya kuanza kutoza, kupunguza, kuongeza au kusamehe viwango vya kodi, ada au tozo zilizopo
- Uboreshaji au uondoaji wa vivutio vya kodi visivyo na tija
- Mapendekezo kuhusu namna bora ya utozaji na usimamizi wa kodi, ada na tozo mbalimbali

Cha kuvutia zaidi, mfumo huu huruhusu mtu kuwasilisha maoni zaidi ya moja kwa kodi au sekta tofauti, hivyo kuongeza wigo wa ushiriki na ufanisi katika uchambuzi wa maoni hayo.

### Faida na Mafanikio Tangu Kuanzishwa kwa Mfumo

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, tangu kuanzishwa kwa Maoni Portal, kumekuwa na ongezeko kubwa la ushiriki wa wananchi na taasisi katika kutoa maoni kuhusu maandalizi ya bajeti ya Serikali. Maoni yanawasilishwa kwa wakati, yanachambuliwa kwa haraka, na hivyo, kuisaidia serikali kutengeneza sera zinazozingatia uhalisia wa mazingira ya kiuchumi na mahitaji ya jamii.

Mbali na hayo, mfumo huu umeondoa vikwazo kwa wananchi wa kawaida, hasa walioko vijijini na kwenye maeneo ambayo yana mtandao, ambao sasa wanaweza kushiriki moja kwa moja bila kuhitaji msaada wa kitaalamu au kusafiri hadi mijini. Aidha, pale ambapo msaada wa kitaalamu huitajika, maofisa wa Wizara ya Fedha kupitia namba za simu zinazotolewa kwenye tangazo la kupokea maoni, hutoa maelezo ya kina ili kuwezesha wadau kuwasilisha maoni hayo kutokea kwenye maeneo waliyopo.

### Mifano ya Maoni Yaliyoleta Mabadiliko Halisi

Mfano halisi wa mafanikio ya mfumo huu ni mapendekezo yaliyowasilishwa na wakulima kuhusu uondoaji wa baadhi ya kodi na tozo kwenye pembejeo za kilimo maoni yaliyowasilishwa na wawekezaji kuhusu utoaji wa vivutio vya kikodi na uongezaji wa viwango vya kodi kwenye baadhi ya bidhaa zinazoingizwa nchini ili kulinda viwanda vya ndani pamoja na maoni yaliyowasilishwa na wafanyabiashara kuhusu utozaji wa ushuru wa huduma (service levy). Maoni hayo yalizingatiwa na kujumuishwa kwenye mabadiliko ya sheria yaliyofanyika katika mwaka husika, jambo linalothibitisha kuwa, sauti ya mwananchi sasa inasikika, na zaidi ya hapo – inafanyiwa kazi kwa njia rasmi na za uwazi.

### Maoni Portal: Ukombozi wa Kidijitali kwa Demokrasia ya Kiuchumi

Mfumo huu wa Maoni Portal haupaswi kuangaliwa tu kama jukwaa la kiteknolojia, bali ni nguzo ya demokrasia ya kiuchumi, inayowezesha kila Mtanzania awe mkulima, mtumishi, mfanyabiashara, mwalimu, au mtaalam kutoa mchango wake katika ujenzi wa taifa kwa njia ya uwazi, sahihi, salama, na ya moja kwa moja.

Katika ulimwengu wa leo unaotawaliwa na mifumo ya kidijitali na matumizi ya takwimu katika kufanya maamuzi, hatua hii ya Wizara ya Fedha ni ushahidi kuwa Serikali imejipanga kwa mageuzi ya kiutendaji yanayotoa sauti kwa wananchi katika kupanga vipaumbele vya mapato na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

### Daraja la Mawasiliano Kati ya Serikali na Wananchi

Maoni Portal si tu mabadiliko ya mfumo, bali ni daraja muhimu linalounganisha mamlaka ya kifedha ya Serikali na wananchi wanaotaka kuchangia kwenye maendeleo ya taifa.

Kupitia mfumo huu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeonesha dhamira ya dhati ya kuwahusisha wananchi moja kwa moja katika kupanga bajeti yao kwa kuzingatia kanuni za uwazi, haki, uwajibikaji na usawa. Hii ni hatua ya kujivunia katika safari ya kujenga jamii inayoshirikishwa kikamilifu katika maamuzi ya kiuchumi na kijamii na hivyo kuwezesha kufikia malengo yanayokusudiwa. Hatua hii pia ni chachu ya kuendelea kuhamasisha utekelezaji na utii wa sheria bila shuruti.

***Mwisho***

# MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA ULIVYOGUSA KONA ZOTE ZA MAENDELEO KIUCHUMI.



*Na Asia Singano*

Sheria ya Fedha ni Sheria inayopitishwa na Bunge kila mwaka ikiwa na lengo la kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali ambapo kwa kawaida Sheria hii ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 2025.

Hivi karibuni Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), tarehe 12 Juni, 2025, aliwasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Fedha Na. 11 wa mwaka 2025 na bbadae kupitishwa na Bunge tarehe 24 Juni, 2025, baada ya Bunge kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali ya shilingi trilioni 56.49 kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.

Muswada huu ulikusudia kufanyia marekebisho ya Sheria 33 ili kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali pamoja na taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali.

Marekebisho hayo yalilenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, hususani katika sekta za kimkakati ikijumuisha viwanda, kilimo, ufugaji na uvuvi, uchukuzi na usafirishaji pamoja na sekta za elimu na afya ili kuboresha uzalishaji na kukuza uchumi wa jumla, kukuza ajira na hatimaye kuboresha maisha ya wananchi.

Hatua hizi zilizoletwa na Sheria hiyo zimelenga pia kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya nchi, kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na kuboresha mazingira ya biashara.

Miongoni mwa Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197; Sheria ya Leseni za Biashara, Sura ya 101; Sheria ya Bajeti, Sura ya 439; Sheria ya Korosho, Sura ya 203; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196; Sheria ya Ushindani.

Sheria ya Tozo za Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura ya 365; Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342;

Sura ya 285; Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276; Sheria ya Bima, Sura ya 394.

Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2025; Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290; Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85; Sheria ya Madini, Sura ya 123; na Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124.

Sheria ya Fedha ni Sheria inayopitishwa na Bunge kila mwaka ikiwa na lengo la kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali ambapo kwa kawaida Sheria hii ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 2025.

Sheria nyingine ni pamoja na Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282; Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127; Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura ya 284; Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari, Sura ya 264.

Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348; Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371; Sheria ya Tume ya UKIMWI, Sura ya 379; Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399; Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161; Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438.

Sheria ya Mamlaka na Majukumu na Msajili wa Hazina, Sura ya 370; Sheria ya Reli, Sura ya 170; Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220; Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

Sheria ya Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura ya 365 imerekebishwa kwa kuongeza Shilingi za Kitanzania 1,000 katika tozo inayotozwa kwa kila abiria anayesafiri kwa ndege; na kuwianisha tarehe ya kulipa ada ya huduma za bandari na tarehe ya kuwasilisha ritani kuwa siku ya 20 ya mwezi baada ya kukusanywa kwa ada hiyo. Lengo la marekebisho ni kurahisisha ulipaji na kuboresha usimamizi wa kodi.

Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342 imerekebishwa kwa kuiongezea majukumu Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board - DIB) ya kuweza kuongeza ukwasi kwa njia ya mkopo kwa benki au taasisi ya fedha yenye changamoto ya ukwasi.

Aidha, kupitia utaratibu huo, benki au taasisi ya fedha iliyoongezewa ukwasi itakuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Lengo la marekebisho ni kuipa DIB nguvu na uhalali wa kisheria wa kushiriki kikamilifu, kwa kushirikiana na Benki Kuu, katika kutathmini na kuamua hatua muafaka ambayo inapaswa kuchukuliwa pindi benki au taasisi ya fedha inapokuwa katika hatari ya kufilisika.

Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 imerekebishwa kwa kuipa Benki Kuu ya Tanzania jukumu la kumlinda mtumiaji wa huduma za kifedha na kuongeza masharti ya kuiwezesha Benki Kuu kutekeleza majukumu yake kwa uhuru; kubainisha majukumu ya Bodi ya Benki katika usimamizi wa Benki Kuu, kuongeza idadi ya wakurugenzi wasio watendaji katika Bodi ya Benki.

Kuongeza muda wa kuhudumu wa wajumbe wa Bodi ya Benki na kuweka utaratibu wa kufanya uteuzi wa wajumbe wa Bodi kwa vipindi tofauti ambapo Lengo ni kuongeza ufanisi katika utendaji wa Bodi ya Benki Kuu, kubainisha muundo, ukomo wa muda na majukumu ya Kamati ya Sera ya Fedha na Kamati ya Ukaguzi, ikilenga kubainisha masharti kuhusu Kamati ya Sera ya Fedha na Kamati ya Ukaguzi ili kuchochea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati husika.

Aidha, Sheria hii imerekebishwa kwa kuipa Bodi ya Benki Kuu mamlaka ya kuanzisha kamati nyingine kwa ajili ya kuiwezesha kutekeleza majukumu yake; kubainisha muda ambao Waziri wa Fedha, anaweza kutoa dhamana ili kurejesha mtaji wa Benki.

Lengo la marekebisho ni kuimarisha ulinzi wa kisheria wa uhuru wa kifedha wa Benki kwa kuweka muda ambao Waziri anaweza kutoa dhamana za Benki ili kuongeza mtaji wa Benki pale inapobidi.

Kubainisha sifa za Maafisa walio katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, uteuzi na muda wa utumishi wa mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani; kuwezesha shughuli za uondoaji na uhamishaji wa fedha (clearing and inter-Financial Institutions transfers) kati ya Taasisi za Kifedha, wakiwemo watoa huduma za fedha kwa njia ya kielektroniki (EMIs), waunganishaji wa malipo (payment aggregators), pamoja na kampuni za teknolojia ya kifedha (FinTechs).

Lengo la marekebisho ni kuwezesha kusomana kwa mifumo ya malipo katika mfumo mzima wa kifedha, kuongeza wigo wa mikopo ya dharura inayotolewa na Benki kwa taasisi za fedha au mabenki kama mkopeshaji wa mwisho; na kuainisha wajibu wa Benki Kuu katika uandaaji wa bajeti ya Serikali, sheria ya fedha na mambo mengine yanayoathiri kazi, mamlaka na wajibu wa Benki Kuu.

Lengo la marekebisho ni kuongeza ushiriki wa Benki Kuu katika nyanja zote zinazohusiana na majukumu ya Benki Kuu.

*Itaendelea...*





# SERIKALI YAENDELEA KUIMARISHA USHIRIKIANO NA WADAU WA MAENDELEO KWA KUIMARISHA UWAJIBIKAJI, UWAZI NA USAWA KWA USTAWI WA JAMII NA UCHUMI WA TANZANIA

*Na Farida Ramadhani*

Ushirikiano wa maendeleo ni mhimili muhimu kwa mataifa yote duniani katika safari ya kujenga ustawi wa kiuchumi, kijamii na kitekenolojia. Ushirikiano huu huchochea kuhamasisha na kuunganisha rasilimali mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Katika muktadha wa Tanzania, ushirikiano huu unajumuisha jitihada za pamoja kati ya Serikali, Washirika wa Maendeleo na Asasi Zisizo za Serikali (AZISE). Kupitia ushirikiano huo, Tanzania imeweza kuongeza rasilimali, kuimarisha ujuzi, kupanua teknolojia, kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi hivyo kupungua umasikini na kuboresha ustawi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Ili kuhakikisha ufanisi wa ushirikiano huo unaendana na vipaumbele vya kitaifa, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilihuisha Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo utakaotumika hadi mwaka 2029/30 (Development Cooperation Framework-DCF wa mwaka 2017/18–2029/30) pamoja na Mpango Kazi wake.

Mwongozo huu unaainisha malengo, mikakati na misingi ya ushirikiano kati ya Serikali na wadau wa maendeleo katika kusimamia utafutaji na matumizi ya rasilimali kwa maendeleo ya Taifa.

Mwongozo huu unaainisha malengo, mikakati na misingi ya ushirikiano kati ya Serikali na wadau wa maendeleo katika kusimamia utafutaji na matumizi ya rasilimali kwa maendeleo ya Taifa. Aidha, umejengwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) kwa Tanzania Bara, na Dira na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar.

Lengo kuu la DCF ni kuratibu ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo, kuoanisha michango yao na mipango ya Taifa, kuweka misingi ya uwazi na uwajibikaji, pamoja na kuratibu ushirikiano wa kimkakati katika maeneo muhimu ya maendeleo. Kama sehemu ya utekelezaji wake, Serikali imehakikisha michango ya wadau hao inajumuishwa kwenye bajeti ya Taifa ili kuongeza uwazi na ufanisi.

Kwa upande wa Asasi Zisizo za Serikali (AZISE), Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum iliandaa Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara.

Mwongozo huu unaainisha majukumu ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, ikiwemo Wizara ya Fedha, ambayo pamoja na mambo mengine ina jukumu la kuhakikisha matumizi ya fedha zinazopokelewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanazingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji.

Aidha, kwa kushirikiana na taasisi nyingine zikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Serikali iliandaa Mwongozo wa Uzingatiaji wa Uwazi wa Masuala ya Kifedha na Ushirikiano kati ya Serikali na Asasi Zisizo za Serikali (Financial Compliance and Engagement Manual for Non-State Actors). Mwongozo huu unakusudia kuwezesha utambuzi wa mchango wa AZISE katika bajeti ya Serikali, kuimarisha misingi ya uwajibikaji na kuhakikisha michango yao inaendana na vipaumbele vya Taifa.

Mwongozo huu ulizinduliwa rasmi Agosti 2025 na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima, kwa niaba ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango. Unalenga kuimarisha ushirikiano wa Serikali na AZISE, kuunganisha nguvu za wadau hawa, na kuhakikisha misingi ya uwazi na uwajibikaji inazingatiwa.

Kupitia mwongozo huu, AZISE zinapaswa kuwasilisha taarifa za shughuli, mapato, matumizi na matokeo ya utekelezaji wa miradi yao ya maendeleo kwa wakati na uwazi, ili kuisaidia Serikali kutambua mchango wao katika maendeleo ya Taifa.

Hatua hii itaimarisha ushirikiano wa Serikali na AZISE, kuboresha huduma kwa wananchi, kudumisha imani ya wahisani, na kuendeleza maendeleo endelevu ya taifa.

***Mwisho***



# UHAKIKI WA WASTAAFU WARAHISISHWA KWA MFUMO WA WASTAAFU KUJIHAKIKI WENYEWE






*Na Peter Haule*

Uhakiki wa Wastaafu ni zoezi linalotumiwa na Serikali kuthibitisha kuwa mtu anayepokea na anayestahiki kupata pensheni pamoja na kuwatambua wastaafu, kufahamu mahitaji yao na kuboresha huduma za ulipaji wa pensheni.

Uhakiki wa wastaafu unahitajika kwa madhumuni mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusaidia kujua idadi sahihi ya wastaafu wanaolipwa na Mfuko husika kila mwezi, kuwezesha Serikali kupanga mipango muhimu kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wastaafu, na kuwezesha Serikali kuwa na taarifa sahihi za kila Mstaafu.

Zoezi la uhakiki uhusisha mstaafu kuwasiliana na mtoa huduma wa pensheni ili kuthibitisha taarifa zake za kibenki, makazi na mawasiliano, utaratibu huu husaidia kuhakikisha usahihi wa taarifa na kuzuia kulipa wastaafu wasio stahili.

Historia ya malipo ya mafao na pensheni kwa Serikali ya Tanzania ilianza kabla ya uhuru wakati wa utawala wa wakoloni, chini ya Serikali ya kiingereza. Sheria zilizotumika Tanganyika kabla ya uhuru zilikuwa katika mfumo wa kurithishwa (Ordinance) kutoka Serikali ya Uingereza.

Sheria ya kwanza nchini ilikuwa ni sheria ya kurithishwa ya Mafao ya Kustaafu ya Waalimu Namba 16 ya mwaka 1925.

Mwaka 1942 Wakoloni walianzisha Mifuko miwili ambayo ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii uliojulikana kama African Provident Fund (APF) na “Government Employees Provident Fund”, Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kuwezesha wafanyakazi wa Serikali ya kikoloni kuweka akiba ya baadaye, Mwaka 1944 Wakoloni walianzisha Mfuko ulioitwa “Native Authorities Provident Fund” (NAPF) ambao ulikuwa ukihudumia watumishi wa mamlaka za wenyeji waliokuwa wakifanya kazi katika mamlaka za wenyeji ikiwemo Machifu wa nyakati za mkoloni.

Baada ya Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 Mfuko ulibadilishwa jina kutoka kuitwa “Native Authorities Provident Fund” na kuanza kuitwa “Local Authorities Provident Fund” (LAPF) na baada ya uhuru Serikali iliendeleza Mifuko hiyo ikilenga kutoa huduma kwa watumishi wa umma na binafsi.

Katika kuendeleza Mifuko hiyo, mwaka 1964 ulianzishwa Mfuko wa National Provident Fund (NPF) uliohusu wafanyakazi wa sekta binafsi na mwaka 1978 ilianzishwa Parastatal Penshens Fund (PPF) ili kuhudumia wafanyakazi wa mashirika ya umma na Mwaka 1999 Serikali ilianzisha Public Service Pension Fund (PSPF) kwa ajili ya watumishi wa umma.

Serikali iliendelea kufanya maboresho ya Mifuko hiyo ambapo mwaka 2018 Serikali iliunganisha baadhi ya Mifuko na kuanzisha Mfuko wa Public Service Social Security Fund (PSSSF) kwa ajili ya watumishi wa umma.

Mfuko huo hutoa Pensheni za kila mwezi au malipo ya mkupuo kwa watumishi na wafanyakazi waliochangia mifuko hiyo wakistaafu kulingana na Sheria na michango, zoezi linaloambatana na uhakiki wa mstaafu huyo ili kuepuka malipo hewa.

Wizara ya Fedha kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali inatoa malipo ya mafao ya hitimisho la kazi kwa wastaafu ambao ni viongozi wa kitaifa, Wanasiasa na watumishi waliostaafu kabla ya Julai, 2004 ambapo hutoa mafao ya kiinua mgongo, pensheni ya kila mwezi, mafao ya mirathi, pensheni ya kifo, mafao kwa wategemezi, mafao ya kiinua mgongo yanayotokana na ajali kazini, pensheni ya ulemavu na mafao ya mkataba.

Wizara ya Fedha katika kuhakikisha ina taarifa kamili na sahihi za Wastaafu wake na inadhibiti malipo ya pensheni kwa wastaafu wasiostahili, imekuwa na zoezi la uhakiki wa Wastaafu hao katika mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani wanaolipwa kupitia Mfumo wa Malipo ya Wastaafu wa Hazina (TPPS) ulioundwa mwaka 2014 ukiwa na kazi ya kuandaa mafao ya hitimisho la kazi na kulipa Pensheni za kila Mwezi.

Ili kutoa huduma nzuri, Wizara iliendelea na maboresho ya zoezi la uhakiki kwa kutengeneza moduli ya uhakiki mwaka 2020 baada ya kubaini kuwepo kwa upungufu wa taarifa kamili za Wastaafu ambapo Wizara ilihitaji kuwafuata wastafu kwenye Halmashauri za Wilaya ili kuwahakiki.

Changamoto ya Moduli hiyo ilikuwa ni pamoja Wastaafu kutumia gharama kubwa kutoka sehemu wanazoishi kwenda Halmashauri au Hazina Ndogo zilizopo mkoani kuhakikiwa.

Pia Serikali ilikuwa inatumia gharama kubwa kuwafuata wastaafu maeneo ya Wilayani na kupoteza muda kutokana na kutekeleza zoezi hilo hivyo kusababisha kutofikiwa kikamilifu kwa lengo la uhakiki.

Katika kutatua changamoto hiyo Mwaka 2025, Wizara ya Fedha iliendelea na maboresho ya Moduli ya uhakiki na kuja na Moduli ya Mstaafu Kujihakiki Mwenyewe (Pensioners Self Verification) utakao muwezesha Mstaafu kujihakiki mwenywe kupitia simu za mkononi na kumuondolea usumbufu wa kusafiri umbali mrefu ili kupata huduma hiyo.

Mfumo huo umeunganishwa na Ofisi ya Vitambulisho vya Taifa, RITA, Benki za Biashara na Hazina ili Mstaafu aweze kujihakiki mwenyewe kwa njia hiyo ya simu ya mkononi lakini pia kupitia Wakala wa mabenki au Ofisi za Hazina Ndogo zote Tanzania Bara.

Mkuu wa Kitengo cha Pensheni Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Bw. Babu Kiguhe akizungumzia Mfumo huo alisema hatua zinazowezesha kujihakiki ni pamoja na Mstaafu kutakiwa kuwa na Kitambulisho cha NIDA kitakachowezesha kutumia namba ya kitambulisho kwenye Simu banking yake pamoja na alama za vidole.



Bw. Kiguhe alisema baada ya kuingiza taarifa hizo benki kupitia mifumo yake italeta taarifa Hazina kisha Hazina wataangalia taarifa za mstaafu kwenye Daftari la Hazina kama yupo na itapeleka taarifa zake NIDA ambao watarudisha taarifa sahihi za mstaafu na mlengwa atapata taarifa kwa Kiswahili kwamba amehakikiwa au la.

Alieleza kuwa iwapo taarifa hazipo sawa Mstaafu ataelekezwa kutembelea Ofisi za Hazina zilizo karibu na yeye kwa ufafanuzi zaidi.

Aidha Bw. Kiguhe alisema Wizara imeunganisha Mfumo huu na Mfumo wa Ofisi ya RITA, Mahakama na Hazina kwa ajili ya kuhakiki taarifa za mstaafu ambaye amefariki ambazo inazipokea kutoka kwa Wasimamimizi wa Mirathi au wategemezi wa marehemu katika kutekeleza zoezi la uhakiki.

Alisema kama Mstaafu anaelipwa Pensheni amefariki, Wategemezi wanatakiwa kuwa na cheti cha kifo kilichotolewa na Ofisi ya RITA kwa ajili ya kusitisha malipo ya pensheni na kuanza kuandaa malipo ya Wategemezi, Cheti hicho kitapaswa kupelekwa Mahakamani ili kufungua Mirathi.

Alisema kuwa wategemezi baada ya kufungua mirathi, Msimamizi wa Mirathi atahitajika kufika Ofisi za Hazina Ndogo na Case reference tu, jambo litakalompunguzia gharama za kudurufu nyaraka mbalimbali; aidha Hazina itaweza kuona taarifa zote na kuanza mchakato wa malipo.

Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande, akijibu swali bungeni kabla ya kuhitimishwa kwa Bunge mwezi Juni, 2025, alisema kuwa Mfumo wa Self Verification utaanza kutumika rasmi baada ya kukamilika kwa taratibu zote ambapo wastaafu watapewa elimu ya namna ya kujihakiki wenyewe na watatangaziwa siku ya kuanza kujihakiki.

Faida za uhakiki wa wastafu sio tu kuthibitisha uwepo na taarifa zao lakini pia husaidia kuzuia malipo hewa kwa kuhakikisha pensheni inalipwa kwa wastaafu halisi na siyo waliofariki au wanufaika kwa majina bandia na kuwa na usahihi wa kumbukumbu zenye kuaminika.

Manufaa mengine ni kupunguza gharama inayotokana na malipo yasiyo halali na uboreshaji wa huduma kwa kuwa takwimu halisi zinawezesha kupanga bajeti na huduma bora zaidi kwa wastaafu.



Uhakiki pia unasaidia kulinda haki za wastaafu kwa kuthibitisha uwepo wao na kutambua iwapo wanastahili kuendelea kulipwa, kuepuka udanganyifu ambao unaweza kufanyika kwa mtu kuchukua mafao au pensheni kwa jina la mstaafu, kuboresha mawasiliano ambapo kupitia uhakiki wastaafu wanaweza kusasisha taarifa zao zikiwemo namba za simu, akaunti ya benki na anwani ili kulipwa kwa wakati.

Faida kwa Serikali na jamii ni pamoja na uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya fedha, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na Serikali kupata picha halisi ya idadi ya wastaafu na hali zao jambo linalosaidia kupanga sera za hifadhi ya jamii.

***Mwisho***

# Kampuni Bora ya Bima ya Jumla kwa Mwaka 2024

SISI NDIYO BIMA

## Shirika la Bima la Taifa (NIC)

Matokeo ya Huduma ya Bima (Faida ya Uandishi) Underwriting Profit




Chanzo:

**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)** Ripoti ya Utendaji wa Soko la Bima kwa Mwaka Ulioishia Disemba 31, 2024

www.tira.go.tz




Tupigie bure: **0800 110 041** @nic_insurance Download on the App Store Google play Pakua **NIC Kiganjani**

VOTED Superbrands EAST AFRICA'S CHOICE 2024-2026

ISO Certified 9001:2015



# WAJIBU WA WAAJIRI KWA WASTAAFU WANAOHUDUMIWA NA HAZINA

*Na Saidina Msangi*

Katika mfumo wa utumishi wa umma, hatua ya kustaafu ni mojawapo ya awamu muhimu inayohitaji maandalizi mazuri ili kuhakikisha kuwa mtumishi anapata mafao yake anayostahili kwa wakati. Mchakato huu hauwezi kukamilika bila ushirikiano wa karibu kati ya taasisi zinazolipa mafao, waajiri na watumishi.

Wizara ya Fedha, kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, inahusika na ulipaji wa mafao kwa watumishi wa Serikali wasiochangia kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, watumishi wa umma waliostaafu kabla ya kuanza kuchangia kwenye Mfuko wa PSPF Julai 1999, Watumishi wa Serikali za Mitaa walioajiriwa kabla ya Julai 1986, Watumishi wa Umma waliohamia kwenye Taasisi kama VETA, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Muhimbili n.k na Viongozi wa Kisiasa (Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wilaya).

Mchakato wa malipo ya mafao na pensheni ya kustaafu hufanyika kwa ushirikiano mkubwa kati ya Hazina na waajiri wa watumishi. Waajiri wana wajibu kuhakikisha nyaraka na vielelezo vingine muhimu vinawasilishwa kwa wakati ili malipo yafanyike.

Tofauti yoyote inayoweza kujitokeza inaathiri mchakato wa malipo na kusababisha ucheleweshwaji wa malipo.

Ni vyema Waajiri kuchukua jukumu hili kwa uzito ili kuondoa kero za malipo ya mafao ambazo zinaweza kujitokeza ikiwemo ucheleweshaji wa malipo.

Makala hii inaangazia wajibu wa waajiri katika mchakato wa maandalizi ya mafao kwa wastaafu wanaohudumiwa na Hazina kwa watumishi wanaotarajia kustaafu ambao mafao yao yatalipwa kupitia Hazina, waajiri wana wajibu maalum kama ifuatavyo:

Majukumu ya waajiri katika mchakato wa maandalizi ya mafao ya wastaafu yamejengwa katika misingi ya sheria ikiwemo Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 (Public Service Act, Cap 298) ambayo inasimamia haki na wajibu wa watumishi wa umma, pamoja na taratibu za kustaafu.

Zoezi la kuchakata taarifa za mtumishi huanza mara baada ya kuajiriwa. Mwajiri na mwajiriwa wana wajibu wa kutunza taarifa za ajira kwa kipindi chote cha ajira ya mtumishi. Nyaraka ni muhimu sana katika uchakataji wa mafao ya kustaafu hivyo basi mamlaka za kulipa mafao zinaweza kuuliza au kuomba nyaraka kwa ajili ya kuchakata mafao ya kustaafu.

Mara nyingi Taasisi zinazohusika na kulipa mafao huomba nyaraka hizi kwa mwajiri na inapotokea zikakosekana kwa sababu yoyote ile mwajiriwa anaweza kurahisisha zoezi kwa kuwasilisha nyaraka alizozitunza.

Moja ya majukumu ya msingi ya mwajiri ni kutunza kumbukumbu zote za utumishi wa kila mtumishi tangu anapoanza kazi hadi siku ya kustaafu.

Kumbukumbu hizi ni pamoja na barua za ajira, barua ya kuthibitishwa kazini, nyongeza za mishahara, uhamisho, mafunzo, likizo, kupandishwa vyeo, hati za mishahara na barua nyingine za kiutumishi.

Aidha, waajiri wanapaswa kuwakumbusha na kuwahamasisha watumishi wao kutunza nyaraka muhimu za utumishi kwa matumizi ya baadaye. Jambo hili ni muhimu sana pale ambapo jalada la mtumishi linaweza kuwa pungufu au limeshapoteza baadhi ya nyaraka. Kwa kufanya hivyo, waajiri wanachangia katika kuharakisha mchakato wa maandalizi na ulipaji wa mafao baada ya mtumishi kustaafu.

Waajiri wanapaswa kutoa elimu na maelekezo kwa watumishi wanaokaribia kustaafu juu ya utaratibu wa malipo ya mafao. Hii ni pamoja na kuwaeleza mafao watakayostahili, aina ya mafao, muda wa kusubiri malipo, na mfuko wa hifadhi ya jamii utakaoshughulikia mafao hayo.

Pia, Waajiri wanapaswa kukusanya majalada yote ya mtumishi anapokaribia kustaafu, kuanzia siku ya kwanza ya ajira hadi siku ya mwisho kazini. Majalada hayo lazima yawe na nyaraka zote muhimu, kisha yawasilishwe Hazina kwa ajili ya hatua zaidi za uchakataji wa mafao.

Aidha, kwa waajiri ambao wanatumia mfumo wa kielektroniki kuingiza taarifa na madai ya hitimisho la kazi wanapaswa kuandaa hesabu za mafao, kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kisha kuziwasilisha Hazina kwa njia ya kielektroniki. Kwa watumishi wa ajira ya kudumu, waajiri wanapaswa kuandaa fomu rasmi ya kustaafu (retiring award), ambayo ni nyaraka muhimu katika kuanzisha mchakato wa malipo ya mafao.

Vilevile, Waajiri wanajukumu la kufanya ukokotoaji sahihi wa mafao ya mstaafu, kwa kuzingatia mishahara, vyeo na muda wa utumishi. Ukokotoaji huu unasaidia kutoa picha halisi ya kiasi stahiki cha mafao.

Waajiri pia wanapaswa kuandaa nyaraka za pensheni na kuwasilisha pamoja na majalada hayo yaliyokamilika kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ajili ya ukaguzi na uthibitisho.

Aidha, kwa wafanyakazi waliopewa ajira za mikataba kabla ya Julai mosi 2024, waajiri hufanya ukokotoaji wa mafao yao na kuwasilisha hesabu kwa CAG kwa ajili ya ukaguzi kabla ya kupelekwa Hazina kwa malipo.

Iwapo mtumishi amefariki kabla ya kustaafu, au baada ya kustaafu lakini taarifa zake za utumishi hazijawasilishwa Hazina na mwajiri, waajiri wanapaswa kupokea nyaraka halali za mirathi kutoka kwa warithi wake, na kuzifikisha Hazina kwa ajili ya kuanza mchakato wa malipo kwa familia au warithi.

Iwapo mtumishi amefariki baada ya kustaafu akiwa anapokea pensheni kutoka Hazina nyaraka za mirathi zitawasilishwa Ofisi za Hazina Ndogo katika mikoa yote ya Tanzania ara na Wizara ya Fedha Zanzibar.

Wajibu wa waajiri kwa wastaafu wanaohudumiwa na Hazina ni wa muhimu sana na unahitaji uwajibikaji, usahihi, na haraka. Utendaji mzuri wa waajiri katika kutekeleza majukumu haya huleta faraja kwa wastaafu kwa kuhakikisha wanapata mafao wanayostahili  kwa wakati.

Kwa hivyo, kila mwajiri anapaswa kuhakikisha kuwa mchakato huu unashughulikiwa kwa umakini wa hali ya juu kwa kuzingatia taratibu zote zilizowekwa kisheria na kiutumishi. Baadhi ya changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza katika utekelezaji wa wajibu huu ni pamoja na kukosekana kwa kumbukumbu kamili za baadhi ya watumishi, uwasilishaji wa nyaraka zisizo sahihi au pungufu, ucheleweshaji wa waajiri katika kuwasilisha nyaraka Hazina au kwa CAG.

Ili kuboresha mchakato wa maandalizi ya mafao kwa wastaafu wanaohudumiwa na Hazina, ni muhimu kuwepo kwa mfumo wa kidigitali wa utunzaji kumbukumbu za watumishi. Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Waajiri na Watumishi kuhusu utaratibu wa maandalizi ya mafao.

Aidha, Wizara ya Fedha imeendelea kutoa miongozo kwa taasisi zote kuhusu nyaraka muhimu na muda wa kuwasilisha pamoja na kuanzishwa kwa timu ya ufuatiliaji ya kimkoa kusimamia utekelezaji wa wajibu huu.

Wajibu wa waajiri katika maandalizi ya mafao ya wastaafu ni jukumu la kisheria, kiutumishi na kijamii. Uwajibikaji, ufuatiliaji na ushirikiano wa karibu kati ya waajiri, Hazina na CAG ni nyenzo muhimu ya kuhakikisha haki za wastaafu zinalindwa.

Kila taasisi ya umma inapaswa kulizingatia hili kwa umakini wa hali ya juu ili kujenga taswira chanya ya utumishi wa umma na kuimarisha ustawi wa wastaafu nchini.

***Mwisho***






# WIZARA YA FEDHA YAIMARISHA UELEWA WA UMMA NA MAFANIKIO YA UCHUMI KUPITIA MAONESHO YA SABASABA

*Na Scola Malinga*

Katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), maarufu kama Sabasaba, yaliyomalizika hivi karibuni, Wizara ya Fedha na Taasisi zake ilishiriki kikamilifu kwa lengo la kuhabarisha umma jukumu lao muhimu la kukuza uchumi wa Taifa.

Ushiriki huo wa Wizara unachangia juhudi za Serikali katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, jambo ambalo ni msingi wa uhuru wa kifedha wa nchi.

Kwa kutoa elimu kuhusu ulipaji kodi, matumizi bora ya fedha za umma na usimamizi wa bajeti, wananchi waliweza kuelewa nafasi yao katika maendeleo ya uchumi wa taifa.

Hili linaendana na lengo la kukuza uchumi jumuishi unaohusisha makundi yote ya jamii, kuanzia wafanyabiashara wadogo hadi wawekezaji wakubwa, katika kuchochea mzunguko wa fedha na fursa za kiuchumi ndani ya nchi.

jamii, kuanzia wafanyabiashara wadogo hadi wawekezaji wakubwa, katika kuchochea mzunguko wa fedha na fursa za kiuchumi ndani ya nchi.

Maonesho haya, yaliyoongozwa na kaulimbiu "Fahari ya Tanzania", yalikuwa jukwaa muhimu la kujieleza kwa Wizara katika kusimamia, kusisitiza na kuwasilisha mchango wake katika maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Takribani watu 10,000 (watu 9,800) walitembelea Banda la Wizara na Taasisi zake, wakiwemo viongozi wakuu wa kitaifa, watendaji mbalimbali wa wizara na taasisi, wakulima, wafanyabiashara wadogo na wakubwa, pamoja na wadau waliojitokeza kwa lengo la kupata elimu na kujifunza kuhusu mafunzo mbalimbali ya kifedha na uchumi.

Ushiriki wa Wizara uliweka mkazo mkubwa katika kuelimisha umma kuhusu huduma za kifedha na usimamizi wa fedha za umma, ukiangazia umuhimu wa ulipaji kodi na matumizi sahihi ya rasilimali na pia namna ambavyo bajeti ya Serikali inavyoweza kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi

Wageni na washiriki kutoka mataifa mbalimbali walioshiriki sabasaba, Wizara iliweza kuwavutia washiriki kuelewa hali ya uchumi wa Tanzania na kuwahamasisha kuwekeza, kufanya biashara, na kushiriki miradi ya maendeleo.

Wizara ilishirikiana na Taasisi 18 zilizo chini yake, ikiwamo Ofisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi (TOST), Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Soko la Bidhaa Tanzania,



Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Chuo cha Usimamizi wa Fedha(IFM).

Taasisi nyingine ni Hazina Sacco Service Ltd, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Benki ya Maendeleo TIB, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania na Taasisi ya Uhasibu Tanzania.

Taasisi hizi zilitoa mafunzo na huduma kama vile ushauri wa kodi, usajili wa malipo, ufahamu wa soko la hisa, uwekezaji, ununuzi wa umma na kupanga mpango madhubuti wa bajeti.

Huduma nyingine zilikuwa namna ya kuanzisha biashara na kuweza kutunza kumbukumbu pamoja na matumizi ya pesa za biashara (mtaji). Hali hiyo yote ilisaidia kuongeza ufahamu na kuunganisha ushirika kati ya Serikali na wananchi waliojitokeza katika maonyesha hayo.

Kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Wizara ya Fedha inaendelea kusisitiza umuhimu wa takwimu sahihi katika kupanga na kutathmini maendeleo ya uchumi wa nchi.

Katika Maonesho ya Sabasaba, wananchi walielimishwa kuhusu namna takwimu za mapato, matumizi, ajira, mfumuko wa bei, na ukuaji wa sekta mbalimbali zinavyotumika katika kupanga bajeti, kufuatilia utekelezaji wa sera, na kupima athari za kiuchumi katika jamii.

Hili linaimarisha uwajibikaji wa Serikali na kuongeza imani ya wananchi katika matumizi ya rasilimali za taifa kwa maendeleo endelevu.

Katika mustakabali wa kutoa elimu kwa umma, Wizara ilishirikiana na Idara mbalimbali zinazowezesha utoaji wa maarifa katika sekta ya fedha na uchumi.

Idara ya Usimamizi wa Madeni ilieleza kwa kina jinsi Serikali inavyodhibiti deni, namna ya kuhakikisha uraia unapata huduma bora na kufahamishwa kuhusu upeo wako katika kulipa deni la Taifa.

Idara ya Uchambuzi wa Sera ilitoa mafunzo kuhusu sera za bajeti, utumiaji wa rasilimali kwa ufanisi, na namna ambavyo mabadiliko ya kiutendo katika sera huathiri uchumi.

Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu iliwasilisha utekelezaji wa malengo ya kitaifa kupitia rasilimali watu, ikibainisha umuhimu wa kuwa na raslimali watu wenye uwezo wa kusukuma mbele mipango ya maendeleo.



Idara ya Mifumo ya Usimamizi wa Fedha na Huduma za Tehama iliwezesha wananchi kupata maelezo kuhusu mifumo ya kisasa kama vile Mfumo wa Malipo ya Serikali (GePG), Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) pamoja na MoFP Repository kwa ajili ya nyaraka rasmi za kifedha na bajeti.

Aidha, Wizara ilitoa elimu kwa umma kuhusu mfumo wa online wa salary slip, mfumo wa kufuatilia michango kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Elimu hizi zilizingatiwa zaidi ili kuwarejesha wananchi kwenye mfumo rasmi wa kifedha wa taifa na kuwasaidia kuelewa kwa undani sera na programu zinazotumika sasa nchini.

Programu za Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) zilizowasilishwa katika maonyesho haya ni kiashiria cha mkakati wa Serikali wa kuchochea uwekezaji wa ndani na nje.

Miradi ya miundombinu kama bandari, usafirishaji wa haraka na majengo ya kibiashara inalenga si tu kuongeza tija katika huduma, bali pia kuunda ajira mpya na kuongeza uzalishaji wa ndani (GDP).

Ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi hiyo unaongeza ushindani wa kiuchumi, kupunguza utegemezi wa fedha za nje na kukuza ustawi wa wananchi kupitia fursa za kiuchumi.

Kituo cha PPP kilitoa maelezo ya kina kuhusu miradi mikubwa ya PPP ambayo ikijumuisha ujenzi wa jengo la biashara Kariakoo chini ya Shirika la Maendeleo la Kariakoo (DDC), miradi miwili ya uendeshaji wa



bandari chini ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), na miradi minne ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART).

Maelezo haya yalieleza nia ya ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi, faida za uwekezaji, na jinsi wananchi wanavyoweza kunufaika moja kwa moja na miradi yenye thamani ya huduma kwa umma. Mafanikio yaliyopatikana kupitia ushiriki huu ni mengi na yenye athari za muda mrefu. Taasisi za biashara zilifanikiwa kuongeza mzunguko wa wateja wapya na kutambulika kwa wingi kwa umma, ikiwa ni alama ya ongezeko la kuaminiwa kwa huduma za kifedha zinazotolewa kupitia Wizara na taasisi zake.

Vyuo vya elimu ya juu vilivyo chini ya Wizara vilivyotembelewa vilinufaika kwa kutoa maelezo kwa wanafunzi watarajiwa na kutambulisha programu mpya za masomo zinazohusiana na masuala ya fedha, uhasibu, utekelezaji wa miradi, ununuzi na ufadhili wa umma. Hii ilileta ufanisi mkubwa katika kuunganishwa kwa watu wanaotaka kujifunza na kupata misaada ya kitaaluma kwa muda mfupi.

Aidha, huduma ya kupewa leseni za udalali ilifanyika kwa wananchi waliokidhi vigezo, hasa wale waliotoka Dar es Salaam ambao walijitokeza kwa kutokujiona nyuma bali wakashiriki kikamilifu katika shughuli za maonesho.

Kupatikana kwa leseni kama hizo kwa wakati mmoja kulionyesha kuwa Wizara imefanikiwa kuimarisha huduma za utekelezaji wa sera kupitia maonyesho kama Sabasaba.

Kutokana na huduma na mpangilio mzuri wa Banda la Wizara ya Fedha, majaji wa maonesho hawakusita kutoa tuzo tatu za ushindi ambapo Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilishinda tuzo ya mshindi wa kwanza, Bodi ya Usimamizi wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) ikashinda tuzo ya nafasi ya pili, na Wizara ya Fedha yenyewe ikashinda tuzo ya mshindi wa tatu.

Hii ilikuwa ni uthibitisho wa uwezo wa taasisi hizi katika utoaji wa huduma bora, ufanisi wa sera na uwezo wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa ununuzi na matumizi ya fedha za umma.

Ushiriki wa wizara katika maonesho ya Sabasaba ni muhimu siyo tu kwa ajili ya mawasiliano na elimu, bali pia katika kuchochea mazingira bora ya kiuchumi, kukuza uwekezaji, na kushirikiana na sekta binafsi kwa maendeleo ya Taifa.

***Mwisho***

Aidha, huduma ya kupewa leseni za udalali ilifanyika kwa wananchi waliokidhi vigezo, hasa wale waliotoka Dar es Salaam ambao walijitokeza kwa kutokujiona nyuma bali wakashiriki kikamilifu katika shughuli za maonesho. Kupatikana kwa leseni kama hizo kwa wakati mmoja kulionyesha kuwa Wizara imefanikiwa kuimarisha huduma za utekelezaji wa sera kupitia maonyesho kama Sabasaba.

Kutokana na huduma na mpangilio mzuri wa banda la Wizara ya Fedha, majaji wa maonesho hawakusita kutoa tuzo tatu za ushindi. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilishinda tuzo ya kwanza, Bodi ya Usimamizi wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) ikashinda tuzo ya pili, na Wizara ya Fedha yenyewe ikashinda tuzo ya tatu. Hii ilikuwa ni uthibitisho wa uwezo wa taasisi hizi katika utoaji wa huduma bora, ufanisi wa sera na uwezo wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa ununuzi na matumizi ya fedha za umma.

Ushiriki wa Wizara ya Fedha katika Maonesho ya Sabasaba umeonyesha kuwa kupitia elimu kwa umma, utoaji huduma kwa wananchi kwa ushirikiano na taasisi mbalimbali, na kupokea maoni na mapendekezo yao, Wizara imeweza kuimarisha mawasiliano na wananchi na kuongeza uwazi katika masuala ya kifedha. Mafanikio haya yameweka msingi imara wa Wizara kuendelea kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali ndani na nje ya Serikali.

Ushiriki wa wizara katika maonesho ya Sabasaba ni muhimu siyo tu kwa ajili ya mawasiliano na elimu, bali pia katika kuchochea mazingira bora ya kiuchumi, kukuza uwekezaji, na kushirikiana na sekta binafsi kwa maendeleo ya Taifa.

***Mwisho***









# UCHUMI WA KIJANI KUKABILIANA NA ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIANCHI

*Na Chedaiwe Msuya*

Katika kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo uharibifu wa mazingira, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, imechukua hatua madhubuti katika kuhakikisha uchumi unakuwa himilivu kwa kutafuta rasimali fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

Rasimali hizo zimetengwa na kutekelezwa kupitia programu na miradi ya maendeleo mbalimbali. Miongoni mwa juhudi zimehusisha kuboresha Sera, Sheria na Mikakati inayohimiza kujenga uchumi wa kijani na kustahimili mabadiliko ya tabianchi.

Aidha katika kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo, Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa mstari wa mbele katika kushughulikia mageuzi ya uchumi wa kijani ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Washirika wa Maendeleo.

Baadhi ya programu na miradi ya maendeleo inayoshughulikia masuala ya mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na Resilience and Sustainability Facility (RSF) chini ya ufadhili kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Catastrophe Deferred Drawdown Option (CatDDO) chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia, Scalling-Up Locally Led Climate Action chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia, Programu ya Economic Competitiveness and Social Inclusion – ECSIP chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika(AfDB), Mradi wa Enhancing Management of State Forest Plantations and Mangrove Forest Reserves in Tanzania kupitia Serikali ya Ufaransa chini ya Shirika lake la Maendeleo (AFD).

## Programu ya Resilience and Sustainability Facility

Resilience and Sustainability Facility (RSF) ni Mfuko wa kifedha ulioundwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ili kusaidia nchi zinazoendelea katika kushughulikia changamoto za muda mrefu kama vile mabadiliko ya tabianchi na maafa ya kiafya kama janga la Uviko 19, ambazo zinaweza kuhatarisha uchumi na jamii kwa ujumla wake.

Malengo ya Programu hii ni kuwezesha mageuzi ya kisera ili kujenga uchumi wa kijani pia uchumi unaoweza kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi hususan katika nyanja za urari wa malipo, upangaji wa bajeti na uwekezaji katika miundombinu himilivu.

Utekelezaji wa programu unahusisha maboresho ya kisera, kisheria, kimuundo na kanuni ndani ya kipindi cha miezi 23 hadi kufikia Machi, 2026. Aidha katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25 Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara za kisekta imefanikisha utekelezaji wa jumla ya maboresho sita ambayo yalihusisha sheria, sera na kanuni na taratibu mbalimbali kama ifuatavyo.

Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (Environment Management Act, 2025 ili kutoa ufafanuzi zaidi wa muundo wa kitaasisi kwa sera zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi

Kuandaa na kuchapisha matukio ya mabadiliko ya tabianchi ya pamoja (climate scenarios) na ramani za athari za mabadiliko ya tabianchi (Vulnerability Maps), na kuingiza hitaji hilo katika mfumo wa upangaji matumizi ya ardhi na usanifu wa ujenzi wa miundombinu.

Kuandaa na kutekeleza mfumo wa Ufadhili wa Hatari za Maafa (Disaster Risk Financing - DRF), kwa kuzingatia matumizi bora ya njia za kujikinga na madhara ya mabadiliko ya tabianchi kabla na baada ya tukio, kwa mujibu wa tathmini ya mahitaji ya DRF, itajumuisha kwa ulinzi wa jamii (social protection).

Kufanya marekebisho ya kanuni za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (Environmental Impact Assessment) ili kujumuisha tathmini za athari za mabadiliko ya tabianchi kwa miradi mikubwa na miradi yote yenye umuhimu wa kimazingira, katika hatua zote za uchambuzi wa mradi.

Kujumuisha matokeo ya tathmini za tabianchi za miradi yote yenye uhusiano na tabianchi katika nyaraka za bajeti zinazowasilishwa Bungeni kuanzia bajeti ya mwaka wa fedha 2025/26, na;

Kujumuisha tathmini ya vihatarishi vya kiuchumi na kifedha zinazotokana na majanga ya asili na mabadiliko ya tabianchi kwenye hotuba ya bajeti.

Wizara imefanikisha kuuanda kijitabu ambacho kinaonesha vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na na kusababisha kutofikiwa kwa shabaha na malengo ya bajeti. Miongoni mwa vihatarishi hivyo ni pamoja na: mabadiliko ya bei za bidhaa muhimu; kuongezeka kwa riba za mikopo; kushuka kwa thamani ya shilingi; madeni sanjari; mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili; migogoro ya kisiasa, uhusiano wa kidiplomasia

### Programu ya Catastrophe Deferred Drawdown Option (CatDDO)

Programu hii inalenga kupata fedha kutoka Benki ya Dunia iwapo dharura itatokea ambapo nchi inaweza kuchukua fedha mara moja baada ya kutangaza kuwa kuna hali ya dharura kutokana na majanga kama vile tetemeko la ardhi, mafuriko, kimbunga, au mlipuko wa magonjwa.

Aidha, Programu hii itawezesha upatikanaji wa fedha za haraka (ndani ya saa 48) pale nchi inapokumbwa na majanga ya asili au ya mabadiliko ya tabianchi au milipuko ya magonjwa kama vile ilivyokuwa Uviko 19.

Aidha Fedha za CatDDO zitazotolewa na Benki ya Dunia kwa masharti kwamba sera za usimamizi wa hatari za majanga zinatekelezwa ipasavyo, na fedha hizi sehemu mojawapo zitatumika kama msaada wa bajeti wa awali, kabla ya misaada au mikopo au misaada mingine kupatikana.

Programu hii pia itaimarisha uwezo wa nchi kujipanga katika kukabiliana mapema na hatari kubwa, kwa kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha kabla na baada ya tukio kutokea.



## Programu ya Scalling-Up Locally Led Climate Action

Serikali kupitia Wizara ya Fedha, imekamilisha uandaji wa programu ya Scalling-Up Locally Led Action yenye lengo la kuongeza utekelezaji wa hatua za kukabiliana na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Programu hii itaimarisha zaidi mifumo ya Serikali Kuu na Serikali za itaa katika kutekeleza mikakati ya kitaifa ya tabianchi na kuendesha shughuli za kuongeza uthabiti wa mabadiliko ya tabianchi zinazoongozwa na jamii katika wilaya mbalimbali nchini. Wakati hatua za kuimarisha mfumo wa kitaifa zitatekelezwa katika ngazi ya kitaifa kupitia taasisi husika za serikali.

Hatua za kuimarisha mifumo ya ngazi ya mitaa na utekelezaji wa shughuli za kuongeza uthabiti wa mabadiliko ya tabianchi zinazoongozwa na jamii zitatekelezwa katika Halmashauri 65 – wilaya 54 kutoka Tanzania Bara na 11 kutoka Zanzibar – zikitoka katika jumla ya wilaya 24. Hii inawakilisha asilimia 30 ya Halmashauri za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na asilimia 100 ya Halmashauri za Zanzibar.

Matokeo yanayotarajiwa kwa muda mfupi ni kuwa na mifumo ya kitaifa ya LLCA (Locally Led Climate Actions) iliyokamilika kwa ajili ya utekelezaji na uhamasishaji wa rasilimali, huku matokeo ya muda wa kati yakilenga kuwa na mifumo ya kitaifa inayowezesha:

Kuimarisha uwezo wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kupokea na kusimamia fedha za tabianchi na kushirikiana na wananchi katika kufanya maamuzi ya pamoja.

Kujenga uhusiano kati ya Serikali za Mitaa na taasisi za kitaifa kwa ajili ya kuboresha ufuatiliaji na tathmini (MRV) ya uwekezaji wa tabianchi.

Kuwezesha uwekezaji wa tabianchi wenye tija na ushirikishwaji kwa jamii katika ngazi ya chini.

Kuongeza uwezo wa nchi kuvutia vyanzo vingine vya fedha za tabianchi.






# Pakua na Soma **majarida ya Hazina Yetu** kupitia Tovuti yetu na Kurasa zetu za Mitandao ya kijamii

Scan Msimbo [QR Code] huu au Tembelea Tovuti
www.mof.go.tz

@mofURT
Wizara ya Fedha

Ministry of Finance-Tanzania

@URTMof
Wizara ya Fedha

@mofURT
Ministry of Finance Tanzania

Wizara ya Fedha Tanzania

@mofURT
Hazina TV - Wizara ya Fedha

UTT AMIS
Asset Management and Investor Services

**MSHIRIKA HAKIKA KATIKA UWEKEZAJI**

# UTT AMIS connect

## Njia rahisi ya kuunganishwa na UTT AMIS

*Kwa Majibu ya papo hapo tumia UTT AMIS CONNECT, AI Namba*

**+255 753 999 113**

Popote ulipo. Wakati wowote.
Rahisi na salama.

***Chukua hatua sasa***



080 011 2020 | www.uttamis.co.tz | UTTAMIS App | Download on the App Store | GET IT ON Google Play

# MATUKIO YALIYOJIRI


















# MAWAZIRI WA FEDHA WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI WAKUTANA ARUSHA KUJADILI KODI NA USHURU

*/ Na Benny Mwaipaja*








Baraza la Kisekta la Mawaziri Wanaosimamia Masuala ya Fedha na Uchumi (SCFEA) wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wamekubaliana kuandaa orodha ya bidhaa zitakazohusika na uondoaji wa kodi na ushuru mbalimbali ikiwa ni utekelezaji wa itifaki ya ushirikiano ili kuchochea biashara na uwekezaji katika Jumuiya hiyo.

Makubaliano hayo yalielezwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ambaye ameongoza Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa Kwanza wa Dharura wa Baraza la Kisekta la Mawaziri Wanaosimamia Masuala ya Fedha na Uchumi (SCFEA) wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliofanyika Makuu ya Jumuiya hiyo, jijini Arusha.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa maelekezo ya Mkutano wa 46 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji (SCTIFI) na makubaliano ya Mawaziri wa Fedha wakati wa mashauriano ya kibajeti katika mikutano yao iliyofanyika mwezi Mei 2025.

Mhe. Dkt. Nchemba alisema kuwa Mkutano huo ulijadili pamoja na mambo mengine, hatua za kikodi zilizo kwenye sheria za fedha za nchi wanachama zenye kuleta athari za kubagua bidhaa zilizozalishwa ndani ya nchi za Jumuiya.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wajumbe kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, wakiwemo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki), Mhe. Dennis Londo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamis Shaaban.




# MKAKATI WA MUDA WA KATI WA UKUSANYAJI MAPATO WAZINDULIWA

*Na. Peter Haule na Joseph Mahumi*

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, amezindua Mkakati wa Muda wa Kati wa Ukusanyaji wa Mapato wa Miaka Mitatu (Medium Term Review Strategy) uliopangwa kutekelezwa kuanzia mwaka 2025/2026 hadi 2027/2028 na Kamati za usimamizi na utekelezaji wa Mkakati huo.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mkakati huo, ukumbi wa Kambarage Wizara ya Fedha, Treasury Square, jijini Dodoma, Dkt. Mwamba alisema kuwa Mkakati huo unalengo la kuweka msingi imara ya ukusanyaji wa mapato, kuweka utabirifu wa sera za mapato na kuongeza makusanyo ya mapato.

Alisema kuwa utekelezaji wa Mkakati huo utasaidia kuongeza uhiari wa ulipaji kodi, kutambua na kuziba mianya ya ukwepaji kodi, kupunguza nakisi ya bajeti na kuimarisha imani ya wananchi na uwekezaji katika mfumo wa mapato.



*Utekelezaji wa kazi hii utaboresha usimamizi wa mapato ya Serikali na kuhakikisha tunakuwa na bajeti endelevu itakayowezesha Serikali kuongeza kasi ya utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi kwa kutumia mapato ya ndani", alisema Dkt. Mwamba.*

Dkt. Mwamba alisema kuwa Mkakati umeainisha maboresho ya mikakati na hatua mbalimbali ambazo zimekuwa zikiendelea kutekelezwa na Serikali katika kuhakikisha Serikali inakusanya mapato mengi kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani.

Alisema kuwa hatua hizo zimegawanyika katika makundi matatu ambayo ni mapendekezo ya maboresho ya sera, maboresho ya usimamizi wa ukusanyaji wa mapato na maboresho ya Sheria.




Dkt. Mwamba alisema kuwa Mkakati huo ulioandaliwa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo washirika wa maendeleo na wadau wengine kutoka taasisi za Serikali na sekta binafsi, unapendekeza kuandaliwa kwa sera ya kodi kitaifa itakayotoa mwongozo wa kuandaa na kuboresha sera za kodi na kuboresha mifumo ya kielektroniki inayotumika katika ukusanyaji wa mapato.

Alisema kuwa Mkakati huo utaongeza utii na uhiari wa ulipaji kodi, kuimarisha na kuboresha usajili wa walipakodi, kuboresha usimamizi wa misamaha ya kodi, kuboresha marejesho ya kodi, kuboresha viwango vya kodi, kuboresha na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na uchumi wa kidigitali na kuboresha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na forodha.

Kwa upande mwingine amewapongeza wajumbe wote walioteuliwa kwa kukubali uteuzi huo ili kushiriki katika kazi hiyo muhimu ambayo imejumuisha wajumbe wenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya uchumi, kodi na fedha kutoka Serikalini na sekta binafsi.

Kwa upande wake Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Sera, Wizara ya Fedha, Dkt. Jonson Nyella, alisema kuwa uandaaji wa Mkakati ulianza na mashauriano yakiongozwa na wataalamu wa ndani na kisha Wataalamu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ambao walitoa msaada wa kiufundi.



Alisema kuwa Mkakati huo ni muhimu katika kupunguza nakisi ya bajeti na hivyo kuwezesha kugharamia miradi ya maendeleo kwa kupitia fedha za ndani, lengo ni kuisaidia nchi kujitegemea ikizingatiwa Nchi imetoka uchumi wa chini kwenda uchumi wa kati ambao unahitaji kujitegemea kwa kiasi kikubwa.



Mwenyekiti wa Kamati iliyozinduliwa ni Katibu Mkuu Hazina na Katibu ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha anayesimamia Uchumi, Wajumbe wa Kamati ni pamoja na Katibu Mkuu Ofisi ya Mipango na Uwekezaji, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi, Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii na Katibu Mkuu Wizara ya Mawasilino na Teknolojia ya Habari.

Wengine ni Gavana wa Benki Kuu, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Msajili wa Hazina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, rais wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) na Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF)

Utaratibu wa kuandaa na kutekeleza Mkakati huo umekuwa ukitumika katika nchi mbalimbali ikiwemo Kenya, Uganda, Malawi, Siera Leone, Ghana, Morocco na Rwanda.








# UCHUMI WA TANZANIA UMEKUA KWA ASILIMIA 5.4 ROBO MWAKA YA KWANZA 2025




*Na. Joseph Mahumi*

Timu ya Wataalamu wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ikiongozwa na Bw. Nicolas Blancher, imemaliza ziara yake nchini Tanzania iliyofanyika kuanzia Septemba 17–24, 2025, ambapo ilifanya tathmini ya mwenendo wa Hali ya uchumi, matarajio ya kiuchumi na utekelezaji wa programu za mageuzi.

Akizungumza Bw. Blancher, katika taarifa iliyochapishwa katika tovuti rasmi ya Shirika hilo, alisema kuwa baada ya ziara yao, wameona uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa thabiti, ambapo umekua kwa asilimia 5.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2025 (kuanzia Julai hadi Septemba), huku mfumuko wa bei ukibaki katika kiwango cha chini cha asilimia 3.4 mwezi Agosti. Sekta za madini, kilimo, viwanda na ujenzi ndizo zimekuwa nguzo kuu za ukuaji huo.

IMF ilibainisha kuwa matarajio Chanya ikiwemo mageuzi ya mapato kupitia Mkakati wa Muda wa Kati wa Mapato (Medium-Term Revenue Strategy) yanatarajiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuwezesha uwekezaji zaidi katika sekta za kijamii.

Aidha, aliongeza kuwa uboreshaji wa soko la fedha za kigeni umeongeza ukwasi na kupunguza tofauti kati ya soko rasmi na lisilo rasmi.

Nakisi ya akaunti ya sasa imeshuka hadi asilimia 2.5 ya Pato la Taifa katika mwaka wa fedha 2024/25, ikichangiwa na mauzo ya madini, bidhaa za kilimo na utalii. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 6.2 kufikia Julai 2025, sawa na miezi minne ya uagizaji bidhaa.

IMF imesisitiza umuhimu wa kuharakisha utekelezaji wa mageuzi ili kufanikisha Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050, ikiwa ni pamoja na kuwekeza kwenye elimu, afya, ajira kwa vijana na mageuzi ya tabianchi kupitia msaada wa washirika wa maendeleo.

IMF inatoa shukrani kwa Serikali ya Tanzania, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na asasi za kiraia kwa ukarimu na majadiliano yenye mafanikio wakati wa ziara hiyo.

> *Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei ndani ya kiwango cha lengo la asilimia 3 hadi 5, na hatua ya kupunguza riba kuu ya benki hadi 5.75% imesaidia kuchochea shughuli za kiuchumi" alisema Bw. Blancher.*



# WAANDAAJI WA BAJETI WATAKIWA KUZINGATIA VIPAUMBELE

*Na. Josephine Majura*



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, amewataka Wataalam wanaoandaa na kusimamia Bajeti ya Serikali kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa miradi ili kuepuka kutekeleza miradi nje ya bajeti iliyopangwa.

Wito huo umetolewa jijini Dodoma wakati akifungua rasmi Kikao kazi cha Wataalam wanaoandaa na kusimamia Bajeti ya Serikali awamu ya pili kuhusu kutumia Mfumo ulioboreshwa wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS) katika kusimamia bajeti na kushauri namna bora ya kutekeleza bajeti zao.

Bw. Mwandumbya alisema kuwa kuna baadhi ya maeneo ambayo wanaomba fedha za kutekeleza miradi nje ya bajeti mwezi mmoja baada ya bajeti kupitishwa jambo ambalo linatia mashaka katika upangaji wa vipaumbele vya utekelezaji wa bajeti.

> *Yawezekana Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi zikawa na mradi wa umwagiliaji ambao utakidhi mahitaji ya mifugo na umwagiliaji lakini utakuta kila mmoja ana mradi wake, hili tunaliona ni changamoto kwa kuwa rasilimali ni zilezile, badala ya kuunganisha kuwa na mradi mmoja hata kama rasilimali itaongezeka kidogo kutakuwa na tija kuliko kila mmoja kutekeleza mradi wake", alieleza Bw. Mwandumbya.*

Katika hatua nyingine aliwataka wataalamu hao kuangalia uwezekano wa kutekeleza miradi inayofanana kwa kushirikiana ili kuepuka kutumia rasilimali nyingi katika eneo moja ili kuleta tija.



Aidha, alisema kuwa mwaka 2026/2027 utakuwa mwaka wenye bajeti inayotokana na vikaokazi vinavyoendeleza na utakuwa mwaka wa kwanza katika utekelezaji Dira ya Taifa ya 2050, hivyo ni vema kuangalia Dira inasemaje ili kuweza kupanga vizuri Bajeti kulingana na Dira hiyo.

Alisema kuwa katika kupanga bajeti ni lazima kuzingatia Dira ya Taifa lakini pia Ilani ya Chama ili kuwa na miradi ambayo inazingatia uelekeo wa nchi katika kipindi cha muda mfupi, wakati na mrefu ili kurahisisha upimaji.









# DKT. NCHEMBA AWASISITIZA WATUMISHI KUSIMAMIA UCHUMI

*Na. Farida Ramadhani*

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amewaagiza viongozi na watumishi wa Wizara hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi na uaminifu ili kuendelea kusimamia uchumi wa nchi.

Alitoa agizo hilo katika Ukumbi wa Mikutano wa Jiji la Dodoma uliopo Mji wa Serikali, Mtumba, wakati wa Kikao cha watumishi wa Wizara hiyo ambacho kinatoa fursa kwa watumishi kukutana kwa pamoja, kukumbushana na kubadilishana uzoefu, taarifa na uelewa kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Serikali kwa ujumla.

Dkt. Nchemba aliwakumbusha watumishi hao kutambua kuwa Wizara ya Fedha ni moyo wa Serikali hivyo ikiyumba tu nchi itayumba na kuleta madhara kijamii na kiuchumi.

Ametoa agizo hilo katika Ukumbi wa Mikutano wa Jiji la Dodoma uliopo Mji wa Serikali, Mtumba, wakati wa Kikao cha watumishi wa Wizara hiyo ambacho kinatoa fursa kwa watumishi kukutana kwa pamoja, kukumbushana na kubadilishana uzoefu, taarifa na uelewa kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Serikali kwa ujumla.

Dkt. Nchemba aliwakumbusha watumishi hao kutambua kuwa Wizara ya Fedha ni moyo wa Serikali hivyo ikiyumba tu nchi itayumba na kuleta madhara kijamii na kiuchumi.

> *Mmekuwa mstari wa mbele kuliwezesha Taifa kuhimili misukusuko ya kiuchumi chini ya uongozi madhubuti wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na usimamizi imara wa uchumi unaendelea licha ya misukosuko inayoendelea duniani", alibainisha Dkt. Nchemba.*



Aliongeza kuwa utendaji wa watumishi wa Wizara hiyo umeiwezesha nchi kutekeleza miradi ya maendeleo lakini pia kuwaongezea sifa binafsi Waziri na Naibu wake Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb).

Dkt. Nchemba alisema Serikali itaendelea kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kufanya vizuri zaidi katika majukumu yao na kuiwezesha nchi kufikia malengo yake.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, aliwaasa Watumishi wa Wizara hiyo kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato na matumizi ya mali na fedha za umma ili kufikia malengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2025/26.

Alisema ni muhimu kwa watumishi hao kutumia weledi na uzoefu walionao kuongeza tija katika usimamizi wa sera, sheria, kanuni na miongozo ya masuala ya fedha na bajeti ili kuwezesha Wizara kutekeleza kwa ufanisi malengo yake na Serikali kwa ujumla.

> *Ninapenda kuwakumbusha watumishi wote kutekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia malengo, shabaha na mpango na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge pamoja na kutunza siri na kuhifadhi nyaraka muhimu za Wizara na Serikali kwa ujumla", alisisitiza Dkt. Mwamba.*

Aliwataka Wakuu wa Idara/Vitengo pamoja na watumishi wote kuzingatia maelekezo hayo kwa ukamilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Naye Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Huduma za Hazina, Bi. Jenifa Christian Omolo alisisitiza umuhimu wa kufanyakazi kwa upendo, umoja na mshikamano pamoja na kuendelea kusimamia maadili ya kazi ili kuwezesha wote kufikia malengo yao.

> *Wote tunategemeana hakuna mtu anayejua kila kitu, hivyo ni muhimu kupeana nafasi ya kuweza kufikia mafanikio yetu, hakuna mtu anayeweza kufanikiwa bila kuwezeshwa", alisisitiza Bi. Omolo.*



Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Usimamizi wa Uchumi, Bw. Elijah Mwandumbya, aliwapongeza watumishi wa Wizara hiyo kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema watumishi wamekuwa wakifanya kazi kwa moyo, kujitolea na kukesha kuhakikisha shughuli mbalimbali za Serikali zinatekelezwa kwa wakati na kwa mafanikio makubwa.



Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo anayesimamia Fedha za Umma, Bi. Amina Khamis Shaaban alisisitiza Wizara hiyo kuendelea kusimamia ukusanyaji wa fedha za ndani ili kuwezesha nchi kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aidha alihimiza watumishi wa Wizara hiyo kusimamia upatikanaji wa mikopo nafuu ili kuiwezesha nchi kutumia fedha hizo kama kichocheo cha kujenga uwezo wa ndani na kujinasua kwenye utegemezi wa muda mrefu.

Bi. Amina aliongeza kuwa katika kupunguza utegemezi huo suala la Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) ni muhimu, na kusisitiza watumishi wa Wizara hiyo hususan wale wanaohusika na PPP kuibua na kusimamia kikamilifu miradi ya ubia.

Kwa upande wao Mhasibu Mkuu wa Serikali CPA (T), Leonard Mkude na Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Bw. Benjamin Magai, walisema kuwa ushirikiano uliotolewa na watumishi umewezesha wizara kukamilisha majukumu ya kimalipo katika mwaka wa fedha 2024/25.

Aidha, waliongeza kuwa miradi mbalimbali ya maendeleo imeweza kutekelezwa pamoja na kukamilisha ufuatiliaji na tathmini katika miradi hiyo.

Katika kikao hicho viongozi walihimiza utulivu, uwajibikaji, uadilifu, kutunza siri na mali za umma pamoja na kujilinda katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Serikali huku wakisisitiza watumishi hao kushiriki zoezi hilo kikamilifu kwa maslahi mapana ya nchi.










# DKT. MWAMBA AISHUKURU IMF KWA KUSAIDIA PROGRAMU ZA MAENDELEO

*Na. Peter Haule na Joseph Mahumi*



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, amelishukuru Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania kuimarisha uchumi kupitia sekta za uzalishaji na huduma za jamii (Extended Credit Facility – ECF) na programu ya kusaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi (Resilient and Sustainability Facility - RSF).

> *Kufikiwa kwa vigezo vya utendaji na kimuundo, kumewezesha IMF kuidhinisha jumla ya dola za Marekani milioni 907.9 ambazo ni takribani asilimia 87 ya fedha za programu ya ECF zilizotolewa tangu kuanza kwake mwaka 2022", alieleza Dkt. Mwamba.*

Dkt. Mwamba ameyasema hayo jijini Dodoma wakati wa Mkutano na Ujumbe wa IMF ukiongozwa na Bw. Melesse Tashu uliofika nchini kwa ajili ya zoezi la kukagua mwenendo wa utekelezaji wa programu ya ECF na RSF.

Dkt. Mwamba alisema kuwa utekelezaji wa programu ya ECF ni wa kuridhisha, ambapo vigezo vya utendaji (Quantitative Performance Criteria) na vigezo vya kimuundo (Structural Benchmarks) vilivyolengwa kufikiwa mwezi Juni, 2025 vimetimizwa kama ilivyopangwa.

Kuhusu programu ya RSF, Dkt. Mwamba alisema kuwa IMF ilitoa kiasi cha dola za Marekani milioni 345.4 katika kutekeleza programu hiyo na tayari Taifa limeanza kunufaika na utekelezaji wake.

Dkt. Mwamba alisema kuwa manufaa hayo yanachangia kwa kiasi kikubwa ndoto za Tanzania kufikia malengo ya kitaifa na malengo ya kimataifa ya Mkataba wa Paris wa mwaka 2015 katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kuwa timu hiyo ya Wataalamu kutoka IMF itakutana na Idara mbalimbali za Serikali ili kujadili maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa programu hizo.

Aidha, Dkt. Mwamba aliahidi kuwa Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa fedha zote zinazotolewa kwa ajili ya programu hizo zinasimamiwa ipasavyo na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake Kiongozi wa Timu ya Wataalamu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Bw. Melesse Tashu, aliipongeza Tanzania kwa kuendelea kuwa mdau mzuri wa Shirika hilo na mtekelezaji mzuri wa miradi ya maendeleo.

Alisema kuwa Tanzania imekuwa ikifanya vizuri katika utekelezaji wa Programu za ECF na RSF jambo ambalo linatoa hamasa kwa mashirika ya kimataifa kuendelea kufanya kazi na Serikali.

Bw. Tashu alisema kuwa Shirika la Fedha la Kimataifa litaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Tanzania ili kuiwezesha kufanikisha miradi muhimu yenye tija kwa wananchi wote na kuhakikisha miradi hiyo inakuwa endelevu kwa kuzingatia mabadiliko ya tabia nchi.

Timu hiyo ya IMF iliambatana pia na Mwakilishi Mkazi wa IMF, Bw. Sebastian Acevedo, katika zoezi hilo litakalofanyika hadi Septemba 24, 2025.











# SERIKALI YALIPONGEZA JKT KWA MATUMIZI MAZURI YA FORCE ACCOUNT

*Na Benny Mwaipaja*

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, amelimwagia sifa na kulipongeza Jeshi la Kujenga Taifa kwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ufanisi mkubwa kupitia mfumo wa Force Account katika Kiteule cha Tanganyika kinachojengwa kupitia Kikosi cha Jeshi hilo cha Milundikwa kilichoko wilaya ya Tanganyika Mkoani Katavi.

Pongezi hizo zilitolewa kwa niaba yake na Kamishna wa Bajeti kutoka Wizara ya Fedha, Bw. Meshack Anyingisye baada ya kutembelea na kujionea utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika Kiteule cha Tanganyika, ambayo ni Kambi tarajiwa ya Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa.

Bw. Anyingisye alisema kuwa uzalendo na nidhamu ya matumizi ya fedha uliooneshwa na Jeshi la Kujenga Taifa katika ujenzi wa majengo mbalimbali katika kiteule hicho ambao hadi kukamilika kwake, mradi unatarajiwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 8.6, unafaa kuigwa na taasisi nyingine za Serikali zinazotekeleza miradi yake kwa njia ya Force Account.

Alisisitiza kuwa utaratibu unaotumiwa na Jeshi la Kujenga Taifa katika ujenzi wa miundombinu yake kwa utaratibu wa matumizi ya fedha bila kutumia zabuni (Force Account), unafaa kuigwa na Taasisi nyingine za Serikali ili malengo ya Serikali ya kuharakisha upatikanaji wa huduma kwa gharama nafuu na kwa ubora wa hali ya juu yaweze kufikiwa.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Rajab Nduku Mabele, Kaimu Mkuu Tawi la Utawala Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa, Kanali Juma Issa Mrai, aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kulipatia fedha Jeshi hilo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo.



Awali, akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kiteule cha JKT-Tanganyika, Mkuu wa Kikosi cha 847 KJ-Milundikwa, Kanali Philemon Mahenge, alisema kuwa Kiteule cha Tanganyika kimepokea kutoka Serikalini kiasi cha shilingi bilioni 2.5 zilizotumika kujenga miundombinu, yakiwemo majengo 9 yanayohusisha utawala, mabwalo, mahanga, zahanati na miundombinu mingine ya Jeshi.

Ziara hiyo ya kutembelea mradi wa Kiteule cha Tanganyika uliwahusisha pia Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali, Wizara ya Fedha, Bw. Japhet Justine, Kamishna wa Sera na Mipango, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Bw. Obed Sayore, Kaimu Mkurugenzi wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Kanali E;phraim Kituhile, Mkurugenzi wa Fedha wa JKT, Luteni Kanali Everine Kibisa na Afisa bajeti Wizara ya Ulinzi, Meja Magreti Kakuru.











# WASHIRIKA WA MAENDELEO KUCHANGIA SH. BILIONI 161 MFUKO WA AFYA WA PAMOJA

*Na. Peter Haule*

Serikali ya Tanzania na washirika wa Maendeleo wanaochangia Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), wamesaini Hati ya makubaliano ya kuchangia katika Mfuko huo kiasi cha dola za Marekani milioni 55.86 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 161.33 kwa mwaka wa fedha 2025/26.

Hafla ya kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano hayo ilifanyika jijini Dar es Salaam kati ya Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha, TAMISEMI na Wizara ya Afya na Washirika wa Maendeleo, wakishuhudiwa na Waziri wa Afya, Mhe. Jenista Mhagama na Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Festo Dugange.

Akizungumza kwa niaba ya Makatibu Wakuu hao, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ambaye pia ndiye Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-maamry Mwamba alisema kuwa makubaliano hayo ya uchangiaji wa fedha kwenye Mfuko wa Pamoja wa Afya ni matokeo ya ushirikiano wa dhati katika kuisaidia sekta ya Afya.

Alisema kuwa misaada hiyo ni mwendelezo wa makubaliano ambayo yalisainiwa mwaka 2021 na yanatarajiwa kumalizika Julai Mosi, 2026 ambapo yataandaliwa makubaliano mengine. kumalizika Julai Mosi, 2026 ambapo yataandaliwa makubaliano mengine.

Dkt. Mwamba alisema, kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawashukuru Washirika hao kwa msaada ambao utasaidia katika juhudi za kuboresha sekta ya Afya.

Alisema kuwa vipaumbele vya misaada hiyo, vinaenda sambamba na vipaumbele vya nchi katika Sekta ya Afya na si katika kukuza sekta hiyo pekee lakini pia misaada hiyo inachochea maendeleo kwa wananchi wengi katika nyanja mbalimbali.

Dkt. Mwamba aliwataja Washirika wa Maendeleo waliochangia katika Mfuko wa Pamoja wa Afya kuwa ni pamoja na Serikali ya Switzerland, Ireland, Canada, Uingereza, Denmark, Korea, Shirika la Kimataifa la Kuwahudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Benki ya Dunia.

Dkt. Mwamba aliahidi kuwa kila msaada utakaotolewa utatumika kwa uwazi na kwa lengo lililokusudiwa ili kuwa na matokeo tarajiwa.

# Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)

TIRA Tumesambaa Nchi Nzima, Tukihakikisha Huduma za Bima Zinakufikia Popote Ulipo!

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Bima Sura ya 394. Chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha, TIRA imepewa majukumu ya kuratibu sera na mambo mengine yanayohusiana na bima katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kazi na majukumu makuu ya Mamlaka ni kukuza na kudumisha soko la bima jumuishi, lenye ufanisi, haki, salama na thabiti kwa manufaa na ulinzi wa wanufaika wa bima. Kazi maalum za Mamlaka zimegawanyika katika maeneo matano makuu ambayo ni:

i) Kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za bima
ii) Kuandaa na kutoa kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia soko la bima
iii) Kulinda haki za mteja wa bima
iv) Kuendeleza na kusimamia uhimilivu na uendelevu wa soko la bima
v) Kuishauri Serikali katika masuala yote yanayohusiana na bima lakini pia

TIRA ni Taasisi ya Kimuungano yenye ofisi zake za makao makuu Tanzania bara Dodoma na Tanzania visiwani Unguja, Zanzibar lakini pia ina Ofisi ndogo ya makao makuu Dar es salaam. Katika kuhakikisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inasogeza huduma ya bima karibu, jumla ya Ofisi za Kanda kumi (10) zimesambaa nchi nzima kuhudumia wananchi na watoa huduma za bima kwa upande wa bara na visiwani kama ifuatavyo:

| Na. | Jina la Kanda | Mikoa inayohudumiwa | Ofisi zilipo |
|---|---|---|---|
| 1 | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | Mbeya, Njombe & Songwe | Mbeya |
| 2 | Kanda ya Kaskazini | Arusha, Kilimanjaro & Tanga | Arusha |
| 3 | Kanda ya Ziwa | Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu & Geita | Mwanza |
| 4 | Kanda ya Mashariki | Dar es Salaam, Pwani & Morogoro | Dar es Salaam |
| 5 | Kanda ya Kati | Dodoma, Manyara & Iringa | Dodoma |
| 6 | Kanda ya Magharibi | Tabora, Shinyanga & Singida | Tabora |
| 7 | Kanda ya Kusini | Mtwara, Lindi & Ruvuma | Lindi |
| 8 | Kanda ya Ziwa Tanganyika | Katavi, Rukwa & Kigoma | Katavi |
| 9 | Kanda ya Unguja | Kaskazini Unguja, Kusini Unguja & Mjini Magharibi | Mjini Magharibi |
| 10 | Kanda ya Pemba | Kaskazini Pemba & Kusini Pemba | Kaskazini Pemba - Chakechake |

TIRA pia tunapatikana katika mitandao mbalimbali ya kijamii; tufatilie katika mtandao wa Instragram; tira_tz, Facebook; Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania; Thread tira_tz lakini pia tufatilie katika tovuti yetu ambayo ni www.tira.go.tz.




# BI. OMOLO APONGEZA UKAMILISHWAJI WA JARIDA LA HAZINA YETU TOLEO LA NNE

*Na Josephine Majura*

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, amekipongeza Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Fedha Kwa kukamilisha Toleo la Nne la Jarida la Hazina Yetu linalozalishwa na Wizara kupitia Kitengo hicho.

Bi. Omolo ameyasema hayo Ofisini kwake Jijini Dodoma wakati wa kupokea Toleo la Nne la Jarida hilo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Fedha, Bw. Benny Mwaipaja, kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, ambalo huandaliwa na Kitengo hicho kila baada ya miezi mitatu.

Alisema kuwa Jarida hilo linamwonekano mzuri na makala pamoja na habari zake zimepangiliwa vizuri.

*Natoa rai kwamba muendelee kuhakikisha Jarida la "Hazina Yetu" linajikita kikamilifu katika kuonesha majukumu ya msingi ya Wizara ya Fedha ikiwemo usimamizi wa sera za fedha, ukusanyaji wa mapato ya Serikali, matumizi ya bajeti, na juhudi za kukuza uchumi wa Taifa" alisema Bi. Omolo*

Alisisitiza kuwa Jarida hilo linapaswa kuendelea kuwa chombo cha kimkakati cha mawasiliano ya Serikali, kinachowasilisha kwa uwazi na kwa lugha rahisi utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, pamoja na mipango ya muda mfupi na mrefu ya Wizara.

Aidha, alielekeza kuwa kila Toleo la Jarida liwe na muundo unaoakisi vipaumbele vya Serikali, likijumuisha makala maalum kuhusu miradi ya kimkakati, mafanikio ya kila robo mwaka, na changamoto zinazoshughulikiwa na Wizara.



Akizungumzia mabadiliko ya kidijitali, Bi. Omolo alieleza kuwa wananchi wa sasa wanategemea kupata taarifa kupitia mitandao ya kijamii, tovuti rasmi za Serikali, na machapisho ya kidijitali, hivyo, Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kiendelee kutumia mikakati madhubuti ya kufikia makundi mbalimbali ya jamii kwa kutumia majukwaa hayo kwa ufanisi.



Katika hatua nyingine, Bi. Omolo alitoa pongezi kwa Kitengo hicho kwa juhudi wanazozifanya katika kuhabarisha wananchi kuhusu majukumu na mafanikio ya Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Bw. Benny Mwaipaja, aliahidi kuongeza juhudi na kuimarisha mbinu za mawasiliano ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu majukumu ya Wizara.



Bw. Mwaipaja alishukuru kwa pongezi zilizotolewa na Naibu Katibu Mkuu Bi. Jenifa Christian Omolo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu Mwamba kwa Kitengo cha Mawasiliano nankwa uwezeshaji wa kufanikisha majukumu ya Kitengo na kuahidi kuwa ushauri na maelekezo yote yaliyotolewa na Naibu Katibu Mkuu yatatekelezwa kikamilifu na kutumika kama mwongozo wa kuboresha zaidi Jarida la "Hazina Yetu" ili liendelee kukata kuu ya kihabari ya wadau wa Wizara.



# WATAALAM WANAOSIMAMIA UAANDAAJI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI WAASWA KUTUMIA KIKAMILIFU MFUMO WA CBMS ULIOBORESHWA ILI KUBORESHA USIMAMIZI WA BAJETI YA SERIKALI

*/ Na. Josephine Majura na Joseph Mahumi*

Wataalam wa wanaoandaa na kusimamia Bajeti ya Serikali wameagizwa kutumia mafunzo ya Mfumo ulioboreshwa wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS), kuboresha utendaji kazi katika usimamizi wa uandaaji na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

Agizo hilo lilitolewa jijini Dodoma na Kamishna wa Bajeti, Wizara ya Fedha, Bw. Meshack Anyingisye wakati akifungua mafunzo ya Mfumo wa CBMS ulioboreshwa na baadae kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2024/25, Maandalizi ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2025/26 na kupata maoni ya kuboresha mchakato wa maandalizi ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/27.

Bw. Anyingisye alisema wataalam hao ni watu muhimu sana katika uandaaji na utekelezaji wa bajeti ya Serikali hivyo watumie mafunzo hayo kusimamia bajeti na kushauri Idara tumizi namna bora ya kutekeleza bajeti zao pamoja na kuboresha usimamzi wa bajeti ya Serikali.

Aidha, alisisitiza kuwa ushiriki wa watumishi hao katika kikao hicho unaashiria kujitolea kwa pamoja katika kuboresha utekelezaji na usimamizi wa bajeti ya Serikali, kuongeza ufanisi katika mchakato wa bajeti na kuhakikisha vipaumbele vya Serikali vinatekelezwa ipasavyo.

Awali akizungumzia mafunzo hayo, Kamishna Msaidizi wa Bajeti anayeshughulikia uchambuzi na mbinu za kibajeti Wizara ya Fedha, Bw. Fundi Makama, alisema mafunzo hayo yamehusisha wadau kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.



*Kamishna Msaidizi wa Idara ya Usimamizi wa Bajeti Wizara ya Fedha, Bw. Fundi Makama, akizungumza wakati wa hafla ya ufunguzi wa Kikao kazi cha Wataalam wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Sekretarieti za Mikoa, kuhusu Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS), jijini Dodoma.*



> “*Usimamizi wa bajeti sio jukumu la Wizara ya Fedha tu, ni jukumu la kila mmoja wetu hivyo ni vema tukatekeleza majukumu yetu kikamilifu katika kushauri na kuchakata takwimu mbalimbali kutoka katika bajeti zetu"*





Alisema mafunzo hayo ya siku tano (5) yatatolewa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza itahusu mafunzo ya Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS) ulioboreshwa na awamu ya pili itajikita kwenye Tathmini ya Uandaaji wa Bajeti ya 2025/26 na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya 2024/25.



Kikao kazi cha wataalam wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Sekretarieti za Mikoa ni jukwaa muhimu la kutafakari na kujadili kuhusu mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25, uandaaji wa bajeti ya 2025/26 na kupata maoni ya maandalizi ya Mwongozo wa uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali wa mwaka 2026/27 ili kubaini maeneo ya kuboresha na kuweka mikakati itakayosaidia kuboresha uandaaji wa mipango na bajeti kwa mwaka 2026/27.





# TANZANIA YAORODHESHWA KATIKA NCHI ZINAZOTAZAMIWA KUFUFUZU KUTOKA NCHI MASIKINI

*Na. Peter Haule na Joseph Mahumi*

Tanzania imeorodheshwa na Kamati ya Sera za Maendeleo ya Umoja wa Mataifa, kuwa miongoni mwa nchi zinazotazamiwa kufuzu kutoka katika kundi la nchi masikini (Least Developed Countries) kwenda nchi inayoendelea.

Hayo yalibainishwa jijini Dodoma na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, wakati wa Mkutano wa Awali wa tathmini ya nchi kutoka nchi maskini kwenda nchi inayoendelea inayofanywa na Umoja wa Mataifa (UN) kupitia Shirika lake la Biashara na Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCTAD).

Dkt. Mwamba alisema hatua hiyo imetokana na Tanzania kupiga hatua kubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika kipindi cha miongo miwili iliyopita kupitia uthabiti wa Sera za uchumi zilizosababisha kukua kwa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.2 kati ya mwaka 2000 na 2024.

> *Pato la mtu kwa mwaka limeongezeka kutoka dola za Marekani 453 mwaka 2000 hadi dola 1,277 kwa mwaka 2023, kiwango cha umasikini uliokithiri kimepungua kutoka asilimia 36 mwaka 2000 hadi asilimia 26 mwaka 2024 kutokana na utekelezaji makini wa sera za fedha na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi", alisema Dkt. Mwamba.*

Dkt. Mwamba alisema kuwa Mfumuko wa bei umeendelea kudhibitiwa na kubaki kwenye tarakimu moja hali iliyoimarisha uthabiti wa uchumi na kuongeza uwezo wa wananchi kukabiliana na gharama za maisha.

Alisema kuwa kumekuwa na uwekezaji wa kimkakati hususani katika miundombinu ya nishati kupitia utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere Hydropower ambao ni mradi mkubwa wa kitaifa wa ujenzi na uzalishaji wa umeme.



Alisema kuwa upo mradi wa usafiri wa abiria na mizigo kati ya Dar es Salaam–Morogoro hadi Dodoma kupitia Reli ya Kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR) na pia miradi ya maboresho katika sekta ya elimu na huduma za afya.

Vilevile alisema kuwa maboresho katika elimu na huduma za afya pamoja na mkazo katika viwanda na ajira yamechangia katika kufikia vigezo vinavyowezesha nchi kuondolewa kwenye kundi la nchi maskini.

Aidha, Dkt. Mwamba ameishukuru Timu ya wataalamu wa Shirika la Biashara na Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCTAD) ambalo limeanza hatua za awali za tathmini ya nchi kutoka nchi maskini kwenda nchi inayoendelea na kuahidi Serikali kutoa ushirikiano thabiti ili kufanikisha zoezi hilo.

Aidha, Dkt. Mwamba alisema kuwa Serikali ina imani na ziara hiyo ya wataalamu wa tathmini kwa kuwa pia itatoa mchango katika maendeleo ya nchi na kusaidia juhudi za Serikali za koboresha sera zitakazoifanya Tanzania kuwa imara zaidi, yenye usawa na mafanikio kwa wote.

Kwa upande wake Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Mhe. Shigeki Komatsubara, alisema kuwa Umoja wa Mataifa upo tayari kuisaidia Tanzania kufanikisha kwa urahisi kuwa katika uchumi wa kati.



Amesema hatua ya sasa ya tathmini ni sehemu ya ushirikiano kati ya Umoja wa Mataifa na Washirika wa Maendeleo na Tanzania.

Kwa niaba ya Umoja wa Mataifa na yeye kama mratibu wa zoezi hilo ni shirikishi litakalosikiliza sauti za watanzania wa rika zote.

Alisema maendeleo yanayotarajiwa yatafikiwa iwapo yatawashirikisha watu wote waliolengwa katika mikakati ya maendeleo.

Mkutano huo ulishirikisha wadau wa taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Asasi zisizo za Serikali na za Kiraia, Washirika wa Maendeleo Tanzania Bara na Zanzibar ambayo yatatumika katika kuandaa tathmini hiyo kwa njia ya mahojiano.



# WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU WASISITIZWA KUZINGATIA UADILIFU

*Na. Saidina Msangi*

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) imehimizwa kuendelea kusisitiza wanachama wake umuhimu wa kuzingatia misingi ya uaminifu na uadilifu katika kazi zao za kila siku ili kuondoa mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali na kuongeza tija na ufanisi katika maendeleo ya nchi.

Rai hiyo ilitolewa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Natu El-maamry Mwamba, wakati wa Mahafali ya 47 ya Bodi hiyo yaliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha APC-Mbweni, Dar es Salaam.

Alisema NBAA inatakiwa kuisaidia Serikali katika kuhakikisha mianya yote ya upotevu wa fedha inadhibitiwa na kuzibwa ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali na hivyo kukuza kasi na ubora wa utoaji wa huduma kwa wananchi.mfumo wa mapato.

> *NBAA inatakiwa kuhakikisha kuwa wahasibu, wakaguzi hesabu na watu wote wanaofanya kazi za uhasibu na ukaguzi hesabu, wanafuata kanuni na miongozo ya uadilifu iliyotolewa na NBAA na pale ambapo itabainika kuwa kuna wanachama wanaokwenda kinyume na kanuni na miongozo hiyo basi hatua kali za kinidhamu zinachukuliwa ili kuwa fundisho kwa wahasibu na wakaguzi wote,"alisema Bi. Omolo.*

Bi. Omolo aliipongeza NBAA kwa ubunifu wa Namba ya Uhakiki Hesabu (NBAA Verification number - NBAAVN) ambayo itasaidia kuweka kumbukumbu za hesabu za fedha vizuri na hivyo kudhibiti mapato ya Serikali na mikopo chechefu kwenye taasisi za fedha.

Aidha, Bi Omolo alisema kuwa kutokana na ugunduzi wa rasilimali za madini, mafuta, na gesi nchini, NBAA inatakiwa kujipanga kuhakikisha nchi inapata wataalamu wa kutosha na wenye ujuzi na weledi unaohitajika katika nyanja ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu za masuala ya madini, mafuta na gesi ili kuleta maendeleo yanayokusudiwa.

Aidha, alisisitiza NBAA kuboresha utendaji wa kazi na utoaji huduma kwa wateja wake ili kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita na kukabiliana na ushindani wa utandawazi.

Pia Bi. Omolo alisisitiza umuhimu kwa NBAA kuongeza wigo wa ufaulu katika mitihani yake na kubuni mbinu mbalimbali za kufanikisha hilo pamoja na kuhakikisha vyuo vinavyoandaa wataalamu vina walimu bora, weledi wa kutosha, vifaa bora vya kufundishia, na mazingira mazuri ya kusomea.

Aliongeza kuwa mbali na kuongeza idadi, mkazo mkubwa lazima uwekwe kwenye kuzalisha wataalamu wenye weledi wa hali ya juu na kuendelea kuzingatia suala la ubora wa wahitimu.

Bi. Omolo alipongeza Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) kwa mchango wake mkubwa katika uandaaji wa bajeti ya Serikali kwa miaka mingi, huku akitaka bodi hiyo kuongeza juhudi katika kuongeza idadi na ubora wa wataalamu wa uhasibu nchini.

Awali akizungumza katika mahafali hayo Mwenyekiti wa Bodi ya NBAA CPA, Prof Silvia Shayo Temu, alisema kuwa NBAA imeanzisha Mfumo wa Namba Maalumu ya Uhakiki wa Taarifa za Hesabu Zilizokaguliwa NBAA (Verification Number - NBAAVN) uliozinduliwa rasmi Julai 1, 2025 kwa ajili ya ukusanyaji na uthibitishaji wa taarifa za hesabu zilizokaguliwa na kuwasilishwa moja kwa moja kwa NBAA

*“Mfumo huu utaongeza uwazi, ufanisi na uhalali wa taarifa za kifedha kwa kuondoa changamoto zilizokuwepo kwenye mfumo wa zamani wa kutumia karatasi, ambao ulikuwa na mianya ya upotoshaji wa taarifa”, alifafanua Prof. CPA Temu.*

Alitoa wito kwa wadau nchini wakiwemo wahasibu, wakaguzi, mashirika ya umma na binafsi kuanza kutumia mfumo huo, na kuwasiliana na NBAA kwa msaada au maelezo ya ziada kwani mfumo huo utabadilisha kwa kiasi kikubwa namna taarifa za kifedha zinavyokusanywa, kuthibitishwa na kutumika kwa kuzingatia uwazi na uwajibikaji.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA CPA Pius Maneno, aliishukuru Wizara ya Fedha kwa ushirikiano mkubwa inaotoa kwa NBAA katika kufanikisha shughuli za kukuza na kuimarisha fani ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu hapa nchini.

Alisema katika mahafali hayo jumla ya wahitimu 1,233 walitunukiwa vyeti katika ngazi mbalimbali ikiwemo Shahada ya Juu ya Uhasibu, ngazi ya cheti, Stashahada ya Viwango vya Kimataifa vya Kihasibu, Stashahada ya Taaluma katika Ukaguzi wa Ndani pamoja na Astashahada ya Viwango vya Kimataifa vya Kihasibu, baada ya kufaulu mitihani yao iliyofanyika miezi ya Novemba, 2024, Februari, 2025, Mei, 2025 na Agosti, 2025.






Tanzania Commercial Bank
1925 - 2025
100
YEARS OF TRUST AND GROWTH
Ishi kidijitali, lipa kidijitali
KAMILISHA HARAKA MALIPO YAKO KIDIJITALI
• Popote Visa Card
• TCB Popote App
• Lipa Popote
• Internet Banking
Kwa maelezo zaidi, tembelea tawi letu jirani nawe au piga 0800 110 160.
Pakua TCB Popote App
Download on the App Store
GET IT ON Google Play
www.tcbbank.co.tz
@Tanzaniacommercialbank

# TANZANIA YAPOKEA MSAADA WA SH. BILIONI 78.6 KUTOKA UJERUMANI

*Na. Peter Haule na Joseph Mahumi*



Tanzania na Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) zimesaini Mikataba mitatu ya misaada yenye thamani ya Euro milioni 25.68 (sawa na sh. Bilioni 78.58) kwa ajili ya miradi ya Maji na Maliasili.

Mikataba hiyo imesainiwa katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba na kwa upande wa Ujerumani imesainiwa na Naibu Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Mhe. Manuel Muller na Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) anaesimamia nchi za Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya, Bw. Christoph Tiskens.

Dkt. Mwamba alisema kuwa mikataba iliyosainiwa ni kwa ajili ya mradi wa programu ya ufadhili wa miradi ya Maji inanayotegemea matokeo (Investment Financing Facility – Output Based Approach (IFF-OBA) kwa kiasi cha Euro milini 10 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 30.6.

Mkataba mwingine ni wa fedha za kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa ustahimilivu wa tabia nchi (Climate Resilient Towns project) kwa kiasi cha shilingi za Tanzania bilioni 2.08.

Alisema kuwa mkataba wa tatu ni wa utekelezaji wa mradi wa Uhifadhi wa Maliasili unaojulikana kama Project for Sustainable Development of Protected Areas kwa kiasi cha Euro milioni 15 sawa na shilingi bilioni 45.9.



Amesema lengo la miradi hiyo ni kutoa motisha kwa Mamlaka za Maji hapa Tanzania kukopa kutoka Benki za Kibiashara kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji ili kuboresha huduma na kuongeza mapato.

Alisema kuwa Kupitia Programu ya IFF – OBA, mamlaka zilizokidhi vigezo zinaweza kukopa kutoka Benki za Biashara na kupatiwa ruzuku kutoka kwenye programu ambapo Mamlaka husika zinapokidhi vigezo, zinaweza kupatiwa ruzuku ya asilimia 50 ya gharama za miradi hadi kufikia kiwango kisichozidi Euro milioni Moja.

Pia mikataba hiyo inalenga uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya Hifadhi za Serengeti na Katavi- Mahale kuhakikisha kunakuwa na uhifadhi na manufaa ya kijamii kwa jamii zinazozunguka hifadhi hizo.

Aidha Dkt. Mwamba ameihakikishia Serikali ya Ujerumani kuwa miradi iliyokusudiwa itatekelezwa kikamilifu na pia Tanzania chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kimaendeleo na Ujerumani kwa manufaa ya watu wa pande zote mbili.

Kwa Upande wake Naibu Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Mhe. Manuel Muller, alisema kuwa utiaji saini wa mikataba hiyo mitatu ambayo ni sehemu ya muendelezo wa ushirikiano wa kifedha kati ya Tanzania na Ujerumani kupitia benki yake ya maendeleo (KfW).



*Ninapenda kuwakumbusha watumishi wote kutekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia malengo, shabaha na mpango na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge pamoja na kutunza siri na kuhifadhi nyaraka muhimu za Wizara na Serikali kwa ujumla", alisisitiza Dkt. Mwamba.*

Naye Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) anaesimamia nchi za Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya, Bw. Christoph Tiskens, alisema kuwa Mikataba hiyo, ni ishara ya hatua nyingine mbele katika ushirikiano kati ya Tanzania na Ujerumani ambao umekuwa mzuri tangu miaka ya 1960.

Bw. Christoph Tiskens alisema kuwa, mikataba hiyo miwili itagusa sekta muhimu sana kwa maendeleo ya Tanzania, kupitia awamu ya pili ya Mfuko wa Uwekezaji wa Fedha kwa ajili ya Miundombinu ya Maji (Investment Financing Facility) yenye thamani ya Euro milioni 10, ambayo itafungua fursa mpya kwa mamlaka za maji hapa Tanzania kupitia benki za ndani.

*Kipengele cha kupitia benki za ndani ni muhimu sana kwa sababu mbinu hii ya ubunifu inasaidia kukuza miradi inayoweza kufadhiliwa (bankable projects) kwa ajili ya mamlaka za maji, hasa katika mazingira ambayo Tanzania inahitaji kiasi kikubwa cha uwekezaji na fedha" alisema Bw. Tiskens.*



Aliongeza kuwa Mkataba wa pili uliouwekwa saini, unaoitwa "Maendeleo Endelevu ya Mfumo wa Ikolojia ya Maeneo ya Hifadhi", utaimarisha ushirikiano wa nchi hizo mbili pamoja na wadau wa hapa nchini, na mkataba huo unalenga kuimarisha uhifadhi wa maliasili ambao ni urithi wa kipekee wa Tanzania na pia kuanzisha minyororo ya thamani kwa ajili ya wananchi wanaoishi karibu na maeneo haya ya asili ya maliasili, ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuleta ajira.





# WIZARA YA FEDHA YAJINOA UTOAJI WA TAARIFA KWA UMMA

*Na. Peter Haule*

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha, Bw. Benny Mwaipaja amewataka wajumbe wa Kamati hiyo kuwa sehemu ya kufanikisha utoaji taarifa sahihi na kwa wakati kwa umma ili kutimiza haki ya wananchi kupata taarifa.

Rai hiyo imetolewa jijini Dodoma wakati wa Kikao kazi cha Kamati hiyo kinachohusisha wajumbe kutoka Idara na Vitengo vya Wizara kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa matumizi ya umma.

Bw. Mwaipaja alisema kuwa Wizara ina jukumu la kutoa taarifa kwa umma kuhusu sera, program, mipango na matukio ya Wizara ili kuuwezesha umma kuwa na uelewa kuhusu majukumu ya Wizara na mambo mengine.

> *Nitoe rai kwa wajumbe wa Kamati hii kuhakikisha mnatoa ushirikiano kwa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Wizara ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa kuainisha kalenda za matukio muhimu kwa umma ili kitengo kiweze kuzifanyia kazi", alisema Bw. Mwaipaja.*

Alisema taarifa zinazopatikana hutumika kuandaa majarida ya Wizara lakini pia kuwezesha kutoa taarifa kupitia Tovuti ya Wizara, Instagram, Whatsap, Tweeter, Linkidin Hazina Tv na vyombo vingine vya Habari kama runinga na magazeti.





Alisema taarifa zinazopatikana hutumika kuandaa majarida ya Wizara lakini pia kuwezesha kutoa taarifa kupitia Tovuti ya Wizara, Instagram, Whatsap, Tweeter, Linkidin Hazina Tv na vyombo vingine vya Habari kama runinga na magazeti.

Alisema kuwa tayari Wizara imetoa Jarida la Hazina Yetu Toleo la Nne ambalo limesheheni taarifa muhimu kwa umma na inaendelea na kuandaa Toleo la Tano ambalo linategemea taarifa zilizopo katika Idara na Vitengo vya Wizara.

Alisema kuwa kupitia chaneli mbalimbali za mawasiliano ambazo Wizara hutumia kuwasilisha Majarida hayo, kuna wadau ambao wanahitaji kuendelea kutoa taarifa kwa kuwa zinaandaliwa kwa lugha nyepesi yenye kueleweka kwa watu mbalimbali.

Aidha, amewataka wajumbe hao kuendelea kuhamasisha wadau wa ndani na nje kufuatilia taarifa zinazotolewa na Wizara kwa manufaa yao katika kuongeza maarifa na matumizi mengine ya tafiti za kitaaluma.














# MPANGO WA MAENDELEO YA SEKTA YA FEDHA WATEKELEZWA KWA UFANISI

*Na. Peter Haule*

Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi wa Sekta ya Fedha na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba ameitaka kamati hiyo kuendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha ulioleta mafanikio katika kukuza upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha, matumizi ya teknolojia na kuimarisha uthabiti wa sekta kwa ujumla.

Hayo yalibainishwa jijini Dodoma, katika Kikao cha Kamati ya Uongozi wa Sekta ya Fedha kilichowakutanisha wajumbe kutoka Wizara zinazohusika na masuala ya Sekta ya Fedha pamoja na Taasisi simamizi kama Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU).

Dkt. Mwamba alisema kuwa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha, inaonesha mweleko chanya wa kufanikisha utekelezaji wa viashiria vya Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha ifikapo 2029/30, hivyo wadau wa sekta ya Fedha wanahamasishwa kuendelea na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha ili kufikia malengo hayo.



Alisema kuwa katika kuhakikisha Sekta ya Fedha inaendelea kuimarika, Wizara itaendelea kuimarisha sekta ya fedha kwa kuongeza juhudi katika uhamasishaji wa matumizi ya mifumo ya malipo ya kidigiti (cashless economy).

Pia itaendelea kuandaa kanzidata ya Sekta ya Fedha ili kurahisisha upatikanaji wa takwimu za sekta ya fedha na kuimarisha ulinzi wa mifumo ya malipo kwa watumiaji na kudhibiti wizi wa kimtandao kupitia wasimamizi wa sekta.

Aidha alisema kuwa Wizara ya Fedha itaendeleza ubunifu wa bidhaa na huduma endelevu katika sekta ya fedha na kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Fedha na kuimarisha uratibu wa masuala ya fedha kwenye jumuiya za Kikanda na Kimataifa.





Kwa upande wake Katibu wa Kamati ya Uongozi wa Sekta ya Fedha na Kamishna Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Bi. Dionisia Mjema alisema kuwa Serikali imetekeleza Mpango Mkuu katika Sekta ya Huduma Ndogo za Fedha kwa kuongeza watoa huduma ndogo za fedha ambapo hadi desemba, 2024 jumla ya taasisi za huduma ndogo zisizopokea amana zilikuwa 2,342, na SACCOS 964 zilipata leseni na vikundi 58,926 vimesajiliwa.

Alisema utoaji wa Elimu ya Fedha katika maeneo ya mijini na vijijini katika mikoa 17 nchini, kuandaa SME Financing Strategy 2023/24 hadi 2028/29, kuandaa mkakati wa ugharamiaji wa miradi ya Maendeleo kwa njia mbadala (APF Strategy).

Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha ni pamoja na ukuaji wa shughuli za sekta ya fedha umeongezeka kwa asilimia 13.8 mwaka 2024, kuongezeka upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha kutoka asimilia 65 mwaka 2017 hadi asilimia 76 mwaka 2023.

Mafanikio mengine ni pamoja na kiwango cha mikopo chechefu kimepungua kufikia asilimia 3.3 mwaka 2024 kutoka asilimia 9.4 mwaka 2020, mchango wa sekta ya fedha kwenye pato la Taifa umeongezeka kufikia asilimia 3.1 mwaka 2024 na kuongezeka kwa mchango wa mikopo kwa sekta binafsi katika pato la Taifa kutoka asilimia 10 mwaka 2021 hadi asilimia 17.2 Juni, 2024.







# WAZIRI MKUU MAJALIWA AFANYA ZIARA OFISI YA SOKO LA HISA DAR ES SALAAM

*Na. Joseph Mahumi*



Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba amesema kuwa Serikali imeweka Sera, Sheria na Taratibu zinazolenga kuchochea biashara, uwekezaji na ukuaji wa uchumi nchini.

Hayo yalisemwa kwaniaba yake na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, akizungumza wakati wa ziara ya Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, katika Ofisi za Soko la Hisa la Dar es Salaam, Morocco, Jijini Dar es Salaam.



*Hatua hiyo ni alama ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, namna ilivyoweka mazingira wezeshi ya kisera, sheria na kiutendaji ikiwa ni msisitizo mkubwa katika kukuza uchumi shirikishi na jumuishi" Alisema Bw. Mwandumbya.*

Aliongeza kuwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilitunga Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2020/21-2029/30 wenye lengo la kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji katika sekta ya umma na binafsi ambapo, Soko la Hisa la Dar es Salaam limeonesha ukomavu wa kuwa jukwaa la kisasa lenye uwazi linalowaunganisha wawekezaji na kampuni zinazohitaji mitaji.

Alisema kuwa hivi sasa DSE imeorodhesha zaidi ya kampuni 28, thamani ya soko (market capitalization) ikiwa imefikia zaidi ya shilingi trilioni 22, na wawekezaji walioko kwenye akaunti wamefikia zaidi ya 683,000, wengi wao wakiwa vijana na wanawake.



*Haya ni mafanikio makubwa yanayoonyesha ukuaji wa mwamko wa wananchi kushiriki katika uwekezaji na kuunganisha uchumi wa familia moja kwa moja na maendeleo ya Taifa" alisema Bw. Mwandumbya.*

Aliongeza kusema kuwa katika kutengeneza mazingira bora ya kufanikisha malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 bado Wizara ya Fedha na DSE wanayo nafasi kubwa ya kupanua wigo wa masoko ya mitaji na dhamana nchini na nje ya mipaka ya Tanzania kwa Kuhamasisha kampuni za bima, benki, kampuni za mawasiliano, na sekta nyingine kuorodheshwa katika soko la hisa ili kukuza mitaji na kuchochea uchumi wa Tanzania.

*Hatua hiyo pia itasaidia kuendeleza bidhaa mpya za kifedha kama hati fungani za kijani (Green Bond) Sukuk, na Mfuko wa uwekezaji wa mali isiyohamishika (Real Estate Investment Trusts-REITs), Kuimarisha mifumo ya kidigitali kama DSE Hisa Kiganjani, ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi ikiwemo diaspora na Kushirikiana na sekta binafsi na wadau wa kikanda kuongeza ushiriki wa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi" Alisisitiza Bw. Mwandumbya.*

Alisema kuwa moja ya maeneo muhimu ni kuimarisha sekta ya fedha na masoko ya mitaji, kwa kuwa ni injini ya kukusanya mitaji ya muda mrefu kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kuthamini mchango wa masoko ya mitaji katika maendeleo na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Akizungumza katika tukio hilo, pamoja na mambo mengine, Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, alitoa rai kwa watanzania kushiriki na kuwekeza katika Soko la Hisa kwa kuwa uwepo wa soko hilo nchini umekuwa chachu ya maendeleo katika nyanja mbalimbali ikiwemo kufungua fursa za uwekezaji wa moja kwa moja kwenye kampuni zenye tija na kuwezesha familia nyingi kupata mapato ya ziada.

Alisema kuwa Soko hilo Kwa wafanyabiashara, limekuwa chanzo cha upatikanaji wa mitaji ya haraka na ya gharama nafuu kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za kibiashara na uboreshaji wa bidhaa na huduma.



*Soko la Hisa limechangia kukuza mapato ya kodi, limeongeza ushiriki wa wananchi katika uchumi, na limeimarisha uthabiti wa sekta ya fedha, zaidi ya hayo, soko limekuwa kichocheo cha kuhamasisha tabia ya uwekezaji na akiba kwa wananchi, jambo ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya muda mrefu ya uchumi wetu" alisema Mhe. Majaliwa.*





DSE
Creating Opportunities

DSE Hisa Kiganjani



# JINSI YA KUANZA KUWEKEZA

## Kuanza kuwekeza ni rahisi sana. Fuata hatua hizi:

1. Pata elimu ya msingi kupitia soko na mawakala wa soko
2. Fungua akaunti ya CDS (Central Depository System) kupitia App DSE Hisa Kiganjani au dalali aliyeidhinishwa na soko
3. Chagua kampuni unayotaka kuwekeza
4. Tuma fedha zako kupitia njia rasmi (benki au simu)
5. Anza kufuatilia maendeleo ya uwekezaji wako

**Hakikisha unatumia taarifa kutoka vyanzo sahihi kama tovuti ya DSE na madalali waliothibitishwa.**

**#SokoLaHisa #FursaZaUwekezaji #DSEHisaKiganjani #KeshoIliyoBora #UjanjaNiKuwekeza**

@dsetanzania

www.dse.co.tz
VISIT OUR WEBSITE

# KONA YA MAONESHO



# WANANCHI WATAKIWA KUFAHAMU MNYORORO WA UGAVI




Wananchi wametakiwa kufahamu mnyororo wa ugavi ambao ni sehemu muhimu yenye mchango mkubwa katika kufanikisha malengo ya Serikali hasa katika nyanja za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Hayo yalisemwa na Afisa Ugavi Mwandamizi kutoka Idara ya Sera za Ununuzi wa Umma, Bi. Vaileth Mwakajisi (wa pili kulia) alipokuwa akitoa elimu kuhusu mnyororo wa ugavi kwa wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha, kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar Es salaam (Sabasaba).

Alisema kuwa mnyororo wa ugavi ni mtangamano wa shughuli za ununuzi, ugomboaji, upokeaji, urejeshaji, utunzaji, uhifadhi na matumizi, usambazaji na uondoaji wa bidhaa, vifaa au mali za umma.

Bi. Vaileth alisema kuwa, mtangamano huo unalenga kutimiza matarajio ya wananchi ya kupata huduma toshelevu na thamani halisi ya fedha zinazotumika katika shughuli za mnyororo huo.

Kwa upande wa wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha walisema kuwa maelezo ya wataalamu na machapisho ya kielimu waliyoyapata bandani humo yamewasaidia kuelewa kwa undani masuala ya mnyororo wa ugavi.






KONA YA MAONESHO SABASABA

# WIZARA YA FEDHA YARAHISISHA UPATIKANAJI WA TAARIFA ZAKE




Wananchi wametakiwa kutumia taarifa zinazotolewa na Wizara ya Fedha kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ili kupata taarifa mbalimbali za uchumi na fedha kwa lengo la kuawasidia kupata ufahamu na maarifa katika kukabiliana na changamoto za kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha, Bi. Eva Varelian, alipokuwa akitoa elimu ya taarifa za uchumi, Sera, fedha na programu za Wizara, kwa wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar Es salaam (Sabasaba).

Alisema kuwa Wizara ya Fedha inazo taarifa nyingi kuhusu uchumi na fedha ambazo zinatolewa kwa wananchi kupitia nyenzo za mawasiliano za Wizara ambapo taarifa hizo zimekidhi vigezo kwa matumizi ya wananchi na taasisi za ndani na nje.

Alisema kuwa Wizara inatumia njia mbalimbali ambazo ni rahisi kwa watumiaji kulingana na mazingira yao, zikiwemo za Whatsap, Mtandao wa X (Tweeter), Linkidin, Hazina Tv, Instagram na Youtube.

Bi. Valerian alisema kuwa Wizara inatoa taarifa kwa njia ya Jarida la Hazina Yetu ambalo hutoka kila robo mwaka na pia inatumia Tovuti ambayo imesheheni taarifa mbalimbali zenye manufaa makubwa kwa wananchi wa hali zote.

Alisema kuwa taarifa za fedha na uchumi ni muhimu katika mipango ya maendeleo kwa wananchi wote wakiwemo wafanyabiashara, wanataaluma, watafiti, wakulima, wawekezaji na wajasiriamali.



KONA YA MAONESHO SABASABA

# WANANCHI WAASWA KUTUMIA NAMBA YA MALIPO WANAPOLIPIA HUDUMA ZA SERIKALI



Wananchi wametakiwa kutumia Namba ya malipo (Control Number) kila wanapofanya malipo ya Serikali ili kuwa na uhakika wa malipo waliyofanya yanafika mahali sahihi kwa ajili ya kutumika katika shughuli mbalimbali za maendeleo zikiwemo za ujenzi wa miundombinu ya afya, elimu na maji.

Hayo yalisemwa na Afisa Mwandamizi kutoka Idara ya Usimamizi wa Mifumo ya Fedha na TEHAMA wa Wizara ya Fedha, Bw. Charles Maganga, alipokuwa akitoa elimu ya matumizi ya namba ya malipo (Control Number) kwa malipo ya Serikali kwa wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar Es salaam (Sabasaba) yenye kaulimbiu ya "Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa Sabasaba, Fahari ya Tanzania".

Alisema kuwa mwananchi mwenye Simu Janja, anaweza kufanya malipo kwa njia ya kupakua GePG App ambayo itampa mwongozo wa ulipaji ambao unaambatana na faida lukuki zikiwemo kuwa na kumbukumbu za malipo na kuweza kupata risiti ya malipo.

Pia Bw. Maganga alisema kuwa kwa wale wanaotumia simu za kawaida wanaweza kufanya malipo kwa kutumia Namba ya Malipo kwa kubonyeza *152*00# kisha kufuata maelekezo njia ambayo ni rahisi kwa watanzania wengi kufanya malipo kwa usahihi.

Alisema Taasisi za Umma, Mashirika na Kampuni zimeunganishwa na Mfumo wa GePG ili kurahisisha ufanyaji wa malipo ya Serikali kwa urahisi, uhakika na uwazi.

Alisema utaratibu wa malipo ni rafiki na hupunguza muda wa kupata huduma kwa kukaa muda mrefu kwenye foleni, utaratibu huo pia unadhibiti mapato, unasaidia kupata taarifa sahihi za mapato ya Serikali kwa wakati.

Bw. Maganga amewahakikishia wananchi kuwa pindi wafanyapo malipo kwa kutumia Namba ya Malipo wawe na uhakika kuwa fedha zao zinafika sehemu iliyokusudiwa kwa ajili ya kutekeleza masuala mbalimbali ya maendeleo yenye kulenga ustawi wa Wananchi na Taifa kwa ujumla.

Amewatahadharisha wananchi kuepuka kufanya malipo ya huduma za Serikali nje ya Namba ya malipo kwa kuwa kunatengeneza mazingira ya watu wasio waadilifu kutumia mwanya huo kutumia fedha kinyume na kusudio la Serikali.



KONA YA MAONESHO SABASABA

# WAZABUNI WATAKIWA KUTUMIA FURSA YA MAONESHO YA SABASABA KUPATA TAARIFA




Wazabuni wanaotaka kufanya kazi na Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma wametakiwa kufahamu Sera, Sheria, taratibu na miongozo mbalimbali ili kuweza kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Hayo yalisemwa na Kamishna wa Idara ya Sera za Ununuzi wa Umma Wizara ya Fedha, Dkt. Frederick Mwakibinga alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha na mabanda mengine kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba) yanayoendelea katika Viwanja vya TANTRADE, Jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa Idara yake ndiyo yenye jukumu la kuandaa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi, kanuni na miongozo inayolenga kukuza ushiriki wa wajasiriamali wadogo na wakati katika masoko ya ununuzi na ugavi katika sekta ya umma.

Dkt. Mwakibinga alitoa rai kwa wananchi kutumia fursa ya Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam kupata taarifa sahihi kuhusu Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ili waweze kushiriki katika zabuni mbalimbali zinazotangazwa na Serikali.

Alisema kuwa ni vigumu kupata taarifa nyingi kwa pamoja lakini kupitia Maonesho hayo, mwananchi anaweza kupata taarifa kikamilifu kupitia Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha ambazo zinahusika katika masuala ya Ununuzi wa Umma na Ugavi.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na Idara yake ni kutengeneza mazingira mazuri katika usimamizi wa mnyororo wa ugavi kupitia Sera ili wananchi wengi waweze kunufaika na mazingira hayo.



KONA YA MAONESHO SABASABA

# WANANCHI WATAKIWA KUPATA ELIMU YA SERA ZA KODI KWA MAENDELEO




Wananchi wametakiwa kuwa na uelewa kuhusu Sera za Kodi zinazoandaliwa na Wizara ya Fedha kwa lengo la kumfanya mwananchi kulipa kodi kwa hiari ili kuisaidia Serikali kutoa huduma bora na endelevu katika sekta mbalimbali ikiwemo ya afya, maji, barabara, nishati na kilimo.

Hayo yalisemwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha na mabanda mengine kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba)

Alisema kuwa Bunge limepitisha Bajeti Kuu ya Serikali ya Kiasi cha shilingi trilioni 56.49 ambayo inalenga pamoja na mambo mengine kutekeleza miradi yenye faida ya moja kwa moja kwa mwananchi kama barabara, nishati, maji na kilimo.

Bi. Omolo alisema kuwa jukumu la mwananchi katika kufanikisha hilo ni pamoja na kulipa kodi kwa hiari kwa mazingira rafiki ambayo yanatokana na Sera nzuri za kodi ambazo zimeandaliwa na Wizara ya Fedha.

Ametoa rai kwa wananchi wanaotembelea katika Maonesho hayo kufika Banda la Wizara ya Fedha ili kukutana na wataalamu ambao watawapa elimu ya Sera ya Kodi na faida zake kwa jamii.

Bi. Omolo amewahakikishia wananchi kupata huduma bora kutoka Serikalini kupitia Bajeti iliyopitishwa na Bunge hivi karibuni kwa kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na kwa gharama nafuu.

Aidha, alisema kuwa ndani ya Banda la Wizara ya Fedha inatolewa elimu ya huduma ndogo za fedha kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa wa masuala ya fedha ili kuondokana na kuchukua mikopo isiyo na tija.



KONA YA MAONESHO SABASABA

# MFUMO WA HAZINA MACHAPISHO WALETA MAPINDUZI YA UPATIKANAJI WA TAARIFA



Mfumo wa Hazina ya Machapisho (MOF Respository) ni muhimu kwa wananchi katika kujua taarifa za uchumi na fedha kuanzia nchi ipate uhuru hadi sasa.

Hayo yalisemwa na Mkutubi Mwandamizi wa Kitengo cha Maktaba Wizara ya Fedha, Bw. Fredy Mpoma, alipokuwa akitoa elimu katika Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba).

Bw. Mpoma alisema kuwa Mfumo huo ambao ni muhimu katika uhifadhi na upatikanaji wa taarifa za Wizara ya Fedha tangu uhuru unasaidia katika kuongeza ufahamu wa wapi uchumi umetoka na unakoelekea kupitia mtiririko wa taarifa mbalimbali.

Alibainisha machapisho yanayopatikana katika Mfumo huo kuwa ni Bajeti, Hali ya Uchumi, Deni la Taifa na Sheria ya fedha tangu uhuru.

Alisema machapisho hayo yanasaidia kuboresha utendaji na ufahamu wa masuala ya uchumi na kuwa na mipango yenye kuzingatia uhalisia kwa kutambua hatua kubwa iliyofikiwa na Serikali katika kuimarisha uchumi hadi sasa.

Alisema kuwa kizazi cha sasa hakina taarifa ya kutosha kuhusu mwenendo wa uchumi tangu uhuru, hivyo kupitia Mfumo huo ni wazi kwamba vijana wanaweza kuwa na hoja za msingi wanapo fuatilia maendeleo ya kiuchumi na hatua ambayo Tanzania imepiga ikilinganishwa na nchi nyingine hususani za Afrika.

Bw. Mpoma alisema kuwa hapo awali ilikuwa vigumu kwa taasisi za elimu ambazo zinajukumu la kufanya tafiti za kitaaluma kupata taarifa kwa usahihi na kwa wakati kuhusu hali ya uchumi na bajeti lakini kwa sasa kwa kutumia mfumo huo imerahisisha kupata taarifa katika kuboresha majukumu yao.



3



WIZARA YA FEDHA

Wizara ya Fedha imeibuka na tuzo ya Mshindi wa Tatu wa jumla kwa upande wa Wizara zilizoshiriki Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba),Jijini Dar es Salaam.

Tuzo hizo zilitolewa na Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Seleman Jaffo ambapo kwa upande wa Wizara ya Fedha Tuzo hiyo imepokelewa na Afisa Habari Mwandamizi, Bw. Ramadhan Kissimba, kwa niaba ya Mkuu wa Kitengo cha Serikalini Bw. Benny Mwaipaja, ambapo ushindi huo ulitokana na Wizara zilizotoa huduma bora kwa wananchi katika Maonesho hayo.


MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA
"SABASABA" FAHARI YA TANZANIA
BRELA






MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA
"SABASABA" FAHARI YA TANZANIA
BRELA

# WAAJIRI WAHIMIZWA KUTUNZA KUMBUKUMBU ZA WATUMISHI KURAHISISHA UTOAJI WA MAFAO




Waajiri wanatakiwa kutunza kumbukumbu za Watumishi wao kuanzia mtumishi anapoajiriwa hadi anapofikisha muda wake wa kustaafu ili kusaidia katika utoaji wa mafao kwa wakati kwa mtumishi anapostaafu.

Rai hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam na Mhasibu Mwandamizi kutoka Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Wizara ya Fedha, Bi. Macelina Haule, alipokuwa akitoa elimu kwa wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba), jijini Dar es Salaam.

Bi. Haule alisema kuwa, Waajiri wanawajibika kuwaelimisha watumishi wanaotarajia kustaafu kuhusu utaratibu wa malipo ya mafao, mafao atakayopata na Mfuko ambao atastahili kulipiwa baada ya kustaafu.

Alisema kuwa wajibu wa Waajiri kwa wastaafu wanaohudumiwa na Hazina ni pamoja na kukusanya majalada yote ya mstaafu kuanzia alipoanza kazi hadi anastaafu na kuhakikisha nyaraka muhimu zimo na kuyawasilisha Hazina.

Bi. Haule alitaja majukumu mengine kuwa ni pamoja na kufanya ukokotoaji wa malipo ya mafao, kuandaa hati ya Pensheni na kuwasilisha majalada yenye hati za pensheni kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Aidha, alisema kuwa Waajiri wanatakiwa kupokea nyaraka muhimu za mirathi kutoka kwa ndugu wa marehemu na kuziwasilisha Hazina kwa ajili ya malipo.





KONA YA MAONESHO
SABASABA

# MWAIPAJA: TUTAENDELEA KUTOA ELIMU KWENYE MAJUKWAA MENGINE BAADA YA SABASABA




Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha, Bw. Benny Mwaipaja amewataka wananchi kuendelea kutumia majukwaa ya Wizara hiyo kujifunza kuhusu uchumi na fedha baada ya kuhitimishwa kwa Maonesho ya Sabasaba kwa mwaka 2025.

Rai hiyo aliitoa jijini Dar es Salaam wakati wa kuhitimisha Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba) katika Viwanja vya Sabasaba, Barabara ya Kilwa.

Bw. Mwaipaja aliwapongeza na kuwashukuru wananchi wote waliopata fursa za kutembelea Banda la Wizara ya Fedha na kujifunza mambo mbalimbali yanayohusu uchumi na fedha na kuahidi kuendelea kutolewa kwa elimu hiyo katika majukwaa mengine.

Alisema Wizara kupitia Idara, Vitengo na Taasisi zake imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutoa elimu kwa weledi kuhusu, Bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge na matumizi yake katika kutekeleza miradi ya maendeleo na Sera ya uchumi ilivyowalenga wananchi katika shughuli zao za maendeleo.

Alitaja mambo mengine yaliyotolewa kwa wananchi kuwa ni elimu ya sekta ya fedha, maktaba, pensheni itolewayo na hazina, miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, mifumo ya fedha, uwekezaji, mabenki, masoko ya bidhaa na mitaji, mnyororo wa ugavi na kozi mbalimbali zinazotolewa na Vyuo vya elimu ya juu vilivyo chini ya Wizara ya Fedha.

Bw. Mwaipaja alisema ubora wa Banda la Wizara na weledi katika kutoa elimu sahihi kwa wananchi kumeifanya Mamlaka ya Uendelezaji Biashara nchini, Tantrade, kutoa tuzo ya ushindi kwa nafasi ya tatu kati ya Wizara zote zilizoshiriki Maonesho hayo ya Mwaka huu, jambo ambalo ni ushindi mkubwa kwa Wizara na Viongozi wanaosimamia weledi wa watumishi ndani ya Wizara na Taasisi zake.



KONA YA MAONESHO NANENANE

# MADALALI WA MINADA WATAKIWA KUJISAJI KIELEKTRONIKI




Wizara ya Fedha imeandaa Mfumo wa Kielektroniki wa utoaji Leseni za Udalali na Uendeshaji minada ya hadhara unaowezesha uombaji na upatikanaji wa Leseni kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia simu za mkononi au kompyuta mpakato ili kuwaondolea wananchi adha na gharama ya kufuata leseni hizo jijini Dodoma.

Akizungumza wakati akitoa elimu kwa wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Nanenane, Jijini Dodoma, Msimamizi wa Mali za Serikali wizarani hapo, Bw. George Killo, alisema Mfumo huo utamuwezesha mwananchi kufanya usajili popote alipo hivyo kupata leseni yake kwa wakati.

"Mwombaji wa leseni ya udalali anapaswa kujisajili kupitia Tovuti ya Wizara ya Fedha (www.mof.go.tz) na kisha kubonyeza kipengele cha GAMIS na kujisajili, kujaza taarifa zinazohitajika, kujaza fomu za maombi kikamilifu na kuwasilisha kwa Katibu Tawala wa Wilaya husika kwa ajili ya uhakiki na Saini," alieleza Bw. Killo.

Alisema mwombaji wa Leseni za Udalali na Uendeshaji Minada ya hadhara anahitajika kuwa na fomu ya maombi iliyojazwa kikamilifu na kugongwa muhuri na Katibu Tawala wa Wilaya husika, Tax Clearance Certificate/incorporation, leseni ya biashara pamoja na Tax Clearance Certificate na viambatisho hivyo viwe katika mfumo wa PDF.

Alisema kupitia mfumo huo mwombaji anaweza kupata taarifa za maombi yake ikiwa yametumwa, yamekataliwa au yamekamilika na waombaji waliofanikiwa wataorodheshwa katika Tovuti ya Wizara ya Fedha na kuchukua leseni zao katika Ofisi ya Usimamizi wa Mali za Serikali katika mikoa yao.

"Leseni hizi zinazotolewa na Wizara ya Fedha zinatumika katika uendeshaji wa minada ya hadhara, ukusanyaji wa madeni, ushuru, tozo, udalali wa mahakama, udalali wa nyumba na viwanja ambapo hutolewa kwa muda wa mwaka mmoja (Januari -Disemba) kwa Sh. 150,000/= na nusu mwaka (Januari – June) (Julai – Disemba) kwa Sh.75,000," alifafanua Bw. Killo.

KONA YA MAONESHO NANENANE

# WASTAAFU WANAOLIPWA NA HAZINA WAASWA KUEPUKA MATAPELI



Wizara ya Fedha imeawaasa wastaafu wanaolipwa mafao na Hazina kujiepusha na jumbe kwa njia ya simu zinazotumwa na watu wasiojulikana zikiwaelekeza kutuma fedha ili kuhakikiwa kwani wanaweza kutapeliwa fedha zao na matapeli hao.

Akizungumza wakati akitoa elimu kwa wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Nanenane, Nzuguni Jijini Dodoma, Afisa Hesabu Mkuu, Kitengo cha Pensheni Wizara ya Fedha Bi. Joyce Chacky, alisema kuwa hakuna zoezi la uhakiki wa wastaafu linalofanywa na Hazina pia hakuna zoezi la uboreshwaji wa pensheni kwa mstaafu mmoja mmoja.

"Siku za karibuni Wizara imekuwa ikipokea malalamiko kadhaa kutoka kwa wastaafu kuombwa fedha kupitia mitandao ya simu ili wafanyiwe uhakiki na kurekebishiwa viwango vya pensheni, hizo taarifa sio sahihi hakuna gharama zozote anazotozwa mstaafu anayehudumiwa na Hazina,"alisema Bi. Chacky.

Alifafanua kuwa Wizara ya Fedha inalipa mafao ya kustaafu na mirathi kwa watumishi waliostaafu wakiwa katika ajira yenye masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni kwa waliokuwa hawachangii kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambao walistaafu kabla ya tarehe 30 Juni, 2004.

Bi. Chacky alisema, hakuna gharama zozote zinazohitajika Wizara ya Fedha kwa ajili ya kushughulikia mafao ya uzeeni na hivyo kusisitiza wasataafu kupuuza jumbe hizo kwa njia ya simu ya mkononi kwani watu hao ni matapeli.

"Tunasisitiza kwa mstaafu anayepokea mafao kutoka kwetu kutoa taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye pale anapoombwa fedha kwa ajili ya kupata huduma yoyote katika ofisi zetu,"alisisitiza Bi. Chacky.

Alitoa rai kwa mteja yeyote mwenye maswali, maoni na madai kufika Ofisi ya Hazina Ndogo iliyopo Mkoani kwake na Wizara ya Fedha, Zanzibar au kupiga simu ya huduma kwa mteja namba 0262160000.

KONA YA MAONESHO NANENANE

# WANANCHI WATAKIWA KUFUATILIA MCHAKATO WA BAJETI ILI KUNUFAIKA KIUCHUMI



Wananchi wametakiwa kujenga utamaduni wa kufuatilia kwa karibu mchakato wa maandalizi ya bajeti ya Serikali ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali za maendeleo katika maeneo yao.

Wito huo ulitolewa na Mchumi Mwandamizi wa Idara ya Bajeti ya Serikali, Wizara ya Fedha, Bw. Eliud Mkiramweni, alipokuwa akitoa elimu kwa wananchi katika Maonesho ya Kilimo ya Nanenane Kitaifa, Viwanja vya Nzuguni, Jijini Dodoma.

Akizungumza katika Banda la Wizara ya Fedha, Bw. Mkiramweni alieleza kuwa bajeti ya Serikali haipaswi kuangaliwa tu kama chombo cha kugharamia shughuli za kiserikali, bali ni dira inayoonesha vipaumbele vya Taifa ambavyo vinaweza kuwanufaisha wananchi kiuchumi.

"Kila mwaka Serikali huandaa bajeti ambayo huainisha maeneo ya kipaumbele kama vile miundombinu, kilimo, afya, elimu, maji, nishati, biashara ndogo na za kati pamoja na mazingira, wananchi wakijua haya mapema, wanaweza kutumia fursa zilizopo kuboresha maisha yao," alisema Bw. Mkiramweni.

Alisisitiza kuwa mchakato wa bajeti ni wazi kwa umma na huanzia ngazi ya kijiji hadi kufikia Bunge, hivyo ni muhimu wananchi wakashiriki katika hatua zote kwa kupendekeza miradi, kufuatilia kiasi cha fedha kinachotengwa, na kuangalia utekelezaji wake.

Aliongeza kuwa ushiriki wa wananchi huongeza uwazi, uwajibikaji na kuibua fursa mpya za kiuchumi hasa kwa vijana, wanawake na wakulima wadogo.

Bw. Mkiramweni alisisitiza kuwa wananchi wanapaswa kujihusisha si tu kwenye mikutano ya kupanga miradi, bali pia kwenye vikao vya halmashauri vinavyohusisha majadiliano ya bajeti, ambapo taarifa muhimu juu ya rasilimali na vipaumbele hutolewa.

Aidha, Bw. Mkiramweni aliwahimiza viongozi wa vijiji na mitaa kuhakikisha wanatoa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa mchakato wa bajeti na kuwashirikisha ipasavyo wananchi wao katika kupanga vipaumbele vya maendeleo.

Aliongeza kuwa uelewa wa bajeti haupaswi kuwa kwa wasomi pekee au maafisa wa Serikali, bali kila Mtanzania mwenye dhamira ya kuona maendeleo katika jamii yake anapaswa kushiriki kikamilifu.

KONA YA MAONESHO NANENANE

# BI. OMOLO APONGEZA WIZARA YA FEDHA NA TAASISI ZAKE KWA UTOAJI WA ELIMU MAONESHO YA NANENANE DODOMA.




Naibu Katibu Mkuu anayesimamia masuala ya Huduma za Hazina, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, alitembelea Banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nanenane, Nzuguni Jijini Dodoma.

Bi. Omolo aliipongeza Wizara na Taasisi kwa kushiriki katika Maonesho hayo yaliyokuwa na kauli mbiu “ChaguaViongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo na Uvuvi2025”, ili kufikisha elimu kwa wananchi hasa katika sekta ya kilimo ili kuchochea ukuaji wa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

‘Hongereni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuelimisha wananchi katika Maonesho haya hakika elimu mnayoitoa italeta tija katika utekelezaji wa majukumu ya wananchi ya kila siku hivyo kuchangia katika ukuaji wa sekta za kilimo, mifugo, uvuvi pamoja na uchumi kwa ujumla”, alisema Bi. Omolo.





**TADB**
*"Benki ya Wakulima"*

# TAMBUA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA **BENKI YA MAENDELEO YA KILIMO**



"Kutoka shambani hadi sokoni" kuimarisha kila hatua ya mnyororo wa thamani wa sekta ya kilimo kwa lengo la kuongeza tija, kuhakikisha ubora wa bidhaa na kuongeza kipato cha mkulima, kuhakikisha ubora wa bidhaa kuongeza kipato cha mkulima, kuhakikisha ubora wa bidhaa kuongeza kipato cha mkulima kupitia utoaji wa mikopo inayohusisha.

| | |
|---|---|
| **PEMBEJEO** | Usambazaji wa mbegu bora, mbolea, na rasilimali nyingine kwa ajili ya uzalishaji. |
| **UZALISHAJI** | Kuwawezesha wakulima kupata vifa, ujuzi, na huduma za fedha ili kuleta tija katika uzalishaji |
| **UHIFADHI** | Kuwawezesha upatikanaji wa madhala, vihenga vya kisasa na vyumba vya barafu ili kutatua tatizo la upotevu wa mazao baada ya kuvuna na kuhakikisha ubora wa bidhaa |
| **UCHAKATAJI** | Kuongeza thamani ya mazai ghafi ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kutumia teknolojia za kisasa ili kuboresha bidhaa |
| **USAMBAZAJI** | Kuongeza ufanisi katika usambazaji wa bidhaa kwenye masoko kupitia njia mbalimbali za usafirishaji |
| **MASOKO** | Kuwezesha upatikanaji wa masoko mapya ya bidhaa za kilimo ili kumuongezea mkulima mapato |

#KILIMOKINABENKIKA

0800 110 120 | www.tadb.co.tz @tadbtz


KAMERA
YETU




*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (Kulia), akimkabidhi Mkakati wa Muda wa Kati wa Ukusanyaji wa Mapato wa Miaka mitatu (Medium Term Review Strategy), Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil, wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mkakati huo ambao umepangwa kutekelezwa kuanzia mwaka 2025/2026 hadi 2027/2028 pamoja na Kamati za usimamizi na utekelezaji wa mkakati huo, katika ukumbi wa Kambarage, Treasury Square, jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Wizara ya Fedha, Bw. Lusius Mwenda (kushoto) na Kamishna Msaidizi wa Idara ya Usimamizi wa Bajeti Wizara ya Fedha, Bw. Fundi Makama, wakiteta jambo wakati wa hafla ya kufunga kikao kazi cha Wataalam wanaoandaa na kusimamia Bajeti ya Serikali kilichofanyika katika ukumbi wa Kambarage, Treasury Square, jijini Dodoma.*



*Mchumi Mkuu kutoka Idara ya Usimamizi wa Bajeti, Wizara ya Fedha, Bw. Boniface Kilindimo (kushoto), akitoa elimu kwa wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha, kuhusu mchakato wa maandalizi ya Bajeti ya Serikali, kwenye Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nanenane, Nzuguni Jijini Dodoma, yenye kauli mbiu "Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo na Uvuvi 2025.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb)(Kulia), akipokea Tuzo Maalamu kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Dodoma, Baba Askofu Dkt. Christian Ndossa, kwa kutambua juhudi zake katika kuwahudumia wananchi, wakati wa halfa ya Uzinduzi wa Harambee ya Ujenzi wa Ofisi Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Dodoma, iliyofanyika katika eneo la mradi-Nzuguni C, Jijini Dodoma.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb) (kushoto), akiteta jambo na Mkurugenzi wa Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Prof. Claver Lumana Pashi (kulia), baada ya kutamatika kwa Mkutano wa Kwanza wa Dharura wa Baraza la Kisekta la Mawaziri Wanaosimamia Masuala ya Fedha na Uchumi (SCFEA) wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), uliofanyika Makao Makuu ya Jumuiya hiyo, jijini Arusha. Katikati ni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, akiagana na Balozi wa Ubeligiji nchini Tanzania, Mhe. Peter Huyghebaert, baada ya mkutano kati yao kuhusu ushirikiano katika sekta mbalimbali za maendeleo kati ya Tanzania na nchi hiyo, uliofanyika, Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, jijini Dar es Salaam.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (Katikati mstari wa mbele), Katibu Mkuu Wizara ya Maji (wa pili kushoto mstari wa mbele), Naibu Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Mhe. Manuel Muller (wa pili kulia mstari wa mbele), na Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) anayesimamia nchi za Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya, Bw. Christoph Tiskens (wa kwanza kushoto mstari wa mbele), wakiwa katika picha ya pamoja na Maafisa waandamizi wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ujerumani, baada ya hafla ya utiaji saini Mikataba mitatu ya misaada yenye thamani ya euro milioni 25.68 (sawa na sh. bilioni 78.58) kwa ajili ya miradi ya maji, mradi wa ustahimilivu wa tabianchi unaojulikana kama "Climate Resilient Towns project" na Uhifadhi wa Maliasili unaojulikana kama "Project for Sustainable Development of Protected Areas", baada ya kusaini hati hizo katika ukumbi wa Hazina Ndogo, jijini Dar es Salaam.*



*Afisa Mwandamizi kutoka Idara ya Usimamizi wa Bajeti, Bw. Boniface Kilindimo, akitoa elimu ya Bajeti kwa , Bw. Etiene Ismail (katikati) na Collins Shirima, walipotembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba) katika Viwanja vya Sabasaba, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.*



*Jaji wa Mahakama Kuu, Mhe. Isaya Arufani Kweka (kulia), Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha, Bw. Benny Mwaipaja (katikati) wakiteta jambo na Afisa Mkuu kutoka Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha Wizara ya Fedha, Bw. Fred Ilomo, alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba), katika Viwanja vya Sabasaba, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.*




*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb)(wa pili kulia), akimkabidhi Tuzo Maalamu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (katikati), wakati alipofungua Kikao Kazi cha Tathimini ya Utendaji kazi cha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, kilichofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC), jijini Arusha,Dodoma. Wengine katika picha ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Bw. Yusuph Mwenda (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya TRA, Bw. Uledi Mussa (wa pili kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Bw. Kenan Kihongosi (wa kwanza kulia).*



*Kamishna wa Bajeti kutoka Wizara ya Fedha, Bw. Meshack Anyingisye, akisalimiana na baadhi ya viongozi wa Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wakati alipotembelea na kujionea utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika Kiteule cha Tanganyika, ambayo ni Kambi tarajiwa ya Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa, iliyoko Wilaya ya Tanganyika Mkoani Katavi.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, akiagana na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF), Prof. Fortunata Makene (kushoto), baada ya kikao kilichofanyika ofisini kwake, Treasury Square, jijini Dodoma.*



*Mchumi Mwandamizi kutoka Idara ya Bajeti, Bw. Samweli Mkwama (Katikati), akimwonesha Mkazi wa jijini Dar es Salaam, Bw. Yahya Rashid (kushoto), namna ya kupakua Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali 2025/26 kupitia msimbo (QR Code), pindi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar Es salaam (Sabasaba) yenye kaulimbiu ya "Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa Sabasaba, Fahari ya Tanzania". Kulia ni Afisa Mwandamizi Idara ya Uchambuzi wa Sera, Wizara ya Fedha, Bw. Lelansi Mwakibibi.*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania Prof. William Pallangyo (kushoto), akiangalia moja ya matoleo ya Jarida la Wizara ya Fedha maarufu kama Hazina Yetu, wakati alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar Es salaam (Sabasaba) yenye kaulimbiu ya "Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa Sabasaba, Fahari ya Tanzania" ambayo yameanza tarehe 28 Juni na kutarajiwa kuhitimishwa Julai 13 mwaka huu. Kulia ni Afisa Habari Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha, Bi. Eva Varelian*



*Afisa Maendeleo Mkuu, Idara ya Uchambuzi wa Sera, Wizara ya Fedha, Bw. Lelansi Mwakibibi, akitoa elimu kwa wakazi wa Dar es Salaam Bi. Salma Khamis (kushoto) na Bi. Joleen Aweda, kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali kwenye Banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba) yaliyofanyika katika Viwanja vya Sabasaba, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Chrisian Omolo, akisikiliza maelezo kutoka kwa Afisa Habari wa Wizara hiyo, Bw. Joseph Mahumi, kuhusu Majarida ya Wizara hiyo (Hazina Yetu) ambayo yanapatikana kwa nakala ngumu na Laini, alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba).*



*Baadhi ya Watumishi wa Wizara ya Fedha walipoungana na maelfu ya wakimbiaji kutoka sehemu mbalimbali katika NBC Marathon 2025 iliyofanyika jijini Dodoma. Ushiriki wao ni ishara ya dhamira ya Wizara katika kuendeleza utamaduni wa kufanya mazoezi na kuimarisha afya ya mwili na akili kwa watumishi wa umma.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), akiteta jambo na Mhasibu Mkuu wa Serikali CPA (T), Leonard Mkude, baada ya kumalizika kwa Kikao cha Watumishi wa Wizara hiyo kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jiji la Dodoma uliopo Mji wa Serikali, Mtumba.*



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil, akisoma Jarida la Hazina Yetu Toleo la Nne la Wizara ya Fedha, katika ofisi za Wizara ya Fedha, Treasury Square, jijini Dodoma.*



*Kamishna Msaidizi Idara ya uendelezaji wa Sekta ya Fedha Wizara ya Fedha, Bi. Dionisia Mjema (Kushoto) na Kamishna wa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU), Bw. Majaba Magana, wakisoma Jarida la Hazina Yetu Toleo la Nne la Wizara ya Fedha, katika ofisi za Wizara ya Fedha, Treasury Square, jijini Dodoma.*




*Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo, akisoma Jarida la Hazina Yetu Toleo la Nne la Wizara ya Fedha, katika ofisi za Wizara ya Fedha, Treasury Square, jijini Dodoma.*

LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA FEDHA
MJI WA SERIKALI - MTUMBA
MTAA WA HAZINA
S.L.P 2802, 40468 DODOMA, TANZANIA
www.mof.go.tz

ISSN 3108-8597
9 773108 859009